# Insha Tatu za Kifalsafa

KAVAZI LA MWALIMU NYERERE
NYERERE RESOURCE CENTRE

# Insha Tatu za Kifalsafa

**Julius K. Nyerere**

**Kavazi Occasional Papers, No. 3**
**2016**

Kimechapishwa na Kavazi la Mwalimu Nyerere
Toleo la kwanza 2016
Chapisho la Pili 2018
Chapisho la Tatu 2019

© Kavazi la Mwalimu Nyerere

ISBN: 978-9976-9903-2-4

Kitabu hiki kimechapishwa kwa hisani ya Rosa Luxembourg Stiftung (RLS)
inayofadhiliwa na Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Ujerumani

Kimechapwa na Inter Press of Tanzania Ltd, Dar es Salaam

# Yaliyomo


| | | |
|---|---|---|
| Utangulizi | Issa G. Shivji | 1 |
| Watu wote ni Sawa? | Julius K. Nyerere | 7 |
| Kazi | Julius K. Nyerere | 22 |
| Kuishi Pamoja | Julius K. Nyerere | 36 |

## Shukrani

Kwanza kabisa ningependa kumshukuru kwa dhati kabisa Ndugu Madaraka Nyerere aliyetoa ushirikiano wake mkubwa kwetu wakati baadhi yetu tulipotembelea maktaba ya Mwalimu Nyerere yaliyoko Butiama. Kwa kweli, kwa kufanya hivyo, Madaraka amedhihirisha kuwa anaelewa kabisa kwamba Mwalimu mwenyewe alitaka nyaraka zake ziwe wazi ili wananchi waweze kuzisoma na kuelewa historia yao.

Pia sinabudi niwashukuru kwa dhati wenzangu Profesa Saida Yahya-Othman na Dakta Bashiru Ally ambao wamejitolea kukifanyia kazi kitabu hiki kwa weledi na umahiri kuhakikisha kwamba machapisho ya Kavazi la Mwalimu Nyerere yanakuwa na ubora wa kisomi wa hali ya juu. Siwezi kumsahau pia Happiness George, Afisa Mtendaji wa Kavazi, ambaye kwa nafsi na nia moja amekuwa anafanya kazi za Kavazi bila kujali muda au maslahi yake. Tuendelee kwa moyo huo kufanya Kavazi liendelee kustahili jina la Mwalimu Nyerere.

Issa G. Shivji
Mkurugenzi
Kavazi la Mwalimu Nyerere
Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia

# Utangulizi

## Falsafa ya Mwalimu Nyerere

Issa G. Shivji*

### Kidokezo

Kitabu hiki kina insha tatu zilizoandikwa na Mwalimu kwa nyakati tofauti na inavyoelekea, kwa sababu mbalimbali. Kadri tunavyojua, makala haya hayajawahi kuchapishwa. Tuliyakuta katika maktaba yake ya Butiama yakiwa karatasi zilizochapwa kwa taipu. Tunayachapisha katika kitabu hiki katika uasilia wake, bila kuyahariri au kuyabadilisha maneno isipokuwa tu kusahihisha zile sehemu ambazo ni wazi zina makosa ya upigaji chapa, kwa mfano, uwekaji nafasi kati ya neno na neno. Ndio maana mara nyingine tunakuta maneno mengine hayapo, ama kwa sababu yalifutika au yalirukwa. Hata hivyo tumeridhika kwamba yanasomeka vizuri na mantiki na malengo yake yanaeleweka kwa ufasaha kabisa. Tunafurahi kupita kiasi kuweka hadharani urathi huu wa Mwalimu. Hazina kama hii ya mawazo, fikra na maandishi mahiri yenye ladha ya kipekee ni nadra sana kupatikana kutoka kwa wanasiasa wa kisasa. Tuna imani kwamba mbali ya kufarijika, kizazi hiki na vizazi vijavyo vitakuwa warithi waaminifu, waadilifu na wabunifu wa lulu hii ya ufahamu na usomi.

### Watu wote ni Sawa?

Insha ya kwanza juu ya *Watu Wote ni Sawa*, ambayo ni ya kipekee katika kueleza msingi wa falsafa ya Mwalimu, tunakisia iliandikwa miaka ya mwisho wa hamsini au mwanzo wa sitini. Tunahisi kwamba lengo lake halikuwa kuichapisha bali lilikuwa kujibainishia [clarify] uelewa wa mwandishi mwenyewe. Kwa maana nyengine, mwandishi alikuwa anahoji

* Mkurugenzi, Kavazi la Mwalimu Nyerere, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia.

dhana na uelewa wake wa usawa kwa jumla, na hasa usawa wa binadamu. Jambo hilo sio geni kwa wanafalsafa. Kabla mwanafalsafa hajatoa maandishi yake hadharani, anajiandikia fikra zake mwenyewe ili kujithibitishia na kujiridhisha kama fikra zake zina mantiki, hazigongani na zina maana aliyoikusudia. Maandishi kama rasimu ndio kioo cha mwandishi kujipima kabla ya kuyawasilisha kwa umma wa wasomaji. Na ndivyo anavyofanya Mwalimu katika maandishi haya juu ya usawa.

Jambo la pili ambalo ningependa nilifafanue ni kuhusu mtindo anaoutumia Mwalimu katika insha hii. Mtindo mojawapo wa falsafa ni kuanza na jambo lililowazi kwa maana ya kwamba linakubaliwa ama kwa hisia au kwa kulielewa bila kuhojiwa au kupingwa. Katika dunia ya leo ukisema kwamba binadamu wote ni sawa, kuna wachache sana watakaokupinga. Isipokuwa ukiwauliza kwa nini wanaamini kuwa binadamu wote ni sawa, wengi hawatakuwa na sababu zaidi ya kusema tu kwamba ni imani yao; wengine wakitoa sababu mbalimbali, zote zikiwa tofauti na hata kupingana, tena kwa kiwango kikubwa tu. Kwa nini inakuwa hivyo? Kwa sababu, ukiangalia juujuu binadamu wote sio sawa, kwa rangi, kwa hadhi, kwa akili, kwa uwezo, kwa vipaji, kwa maumbile n.k. Hata hivyo, bado wengi wana imani kwamba binadamu wote ni sawa pamoja na kwamba macho yao yanawaambia kinyume. Kama kweli jambo linavyoonekana haliendani na kinachoaminika, basi linaibua swali la kifalsafa. Swali la kuchunguzwa na kupatiwa jibu ni hili: Nini kiini cha imani kwamba binadamu wote ni sawa wakati hawaonekani kuwa sawa?

Mwalimu anatumia mtindo huu - kwa kuanza na jambo lenyewe linavyoonekana tofauti na imani ya wengi, anaeleza kwa undani *msingi* na *hoja* ya imani kwamba binadamu wote ni sawa.

Kwa hivyo, sehemu ya kwanza ya makala haya ni kufafanua kwamba binadamu wote sio sawa. Wako warefu na wafupi, weupe na weusi, wake na waume, watu wazima na watoto wachanga, wenye vipaji na wasio na vipaji – lakini wote ni binadamu, wote kwajumla yao ni tofauti na wanyama. Pamoja na tofauti hizo kwa nini tunaendelea kung’ang’ania kwamba binadamu wote

ni sawa? Kipi ni chanzo au msingi wa ubinadamu wa binadamu na unyama wa wanyama? Anaorodhesha na kufafanua tofauti za binadamu, kudhihirisha kwamba watu wote sio sawa kwa ustadi mkubwa kiasi kwamba ukielekea kumaliza kusoma sehemu hii ya kwanza, unaweza ukaanza kuamini kwamba watu wote sio sawa. Katika usomaji wako, ukifikia tu kuanza kuamini hivyo, mwandishi anakugeuzia kibao. Anakurejesha kwenye imani yako ya awali uliyoanza nayo kwamba binadamu wote ni sawa. Anauliza: Baada ya uthibitisho huu kwamba binadamu wote sio sawa na hawaonekani kuwa sawa, kwa nini wengi wetu tunaamini na kutangaza 'binadamu wote ni sawa' na hata kupigania usawa wa binadamu?

Mwandishi sasa anaanza sehemu yake ya pili ya kujenga hoja kwamba watu wote ni sawa. Anajenga hoja yake hatua kwa hatua, msingi kwa msingi, akitofautisha kwa umahiri mkubwa hoja nyepesi na hoja nzito, akijikita kwenye mizizi na kutokwama kwenye visiki. Mwalimu anajenga hoja yake kama msusi anavyosuka nywele, akichota nywele vimacho kwa vimacho. Mfanano ni mfumaji wa sweta aliyebobea na anayefurahia kazi yake - anazungumza, anafurahi, anacheka, anafanya mzaha, mara anakutolea macho kama kwamba anakushangaa au kukulaumu, mara anakupapasa kwa macho kwa upendo unaorahasisha, huku akichota uzi bila kuruka hata nusu hatua.

Yaani, kusoma insha hii ya Mwalimu ni raha tupu! Unatamani kuisoma tena na tena, na tena – hukinai.

## Kazi

Insha ya pili ni juu ya kazi. Hii haikuandikwa bali ni nakala ya mazungumzo na TANU STUDY GROUP. Enzi zile vijana wanazuoni wa TANU walikuwa wanakutana karibu kila Jumapili kujadili, kuzungumza, kufikiri na kufikirishana, wakitoa maoni yao na madukuku yao juu ya masuala ya kijamii, hususan kuhusu safari ya kujenga ujamaa na vizingiti vyake. Mara moja moja Mwalimu alikua anawatembelea na kuzungumza nao, au anavyosema mwenyewe, 'kupiga soga'. Soga mojawapo lilitokea miezi

minne tu baada ya Azimio la Arusha, tarehe 13 Juni 1967. Soga lenyewe likawa juu ya dhana ya kazi.

Mbali na matini juu ya "Kazi" tulioipata Butiama, tumepata pia matini nyengine mbili mahala kwengine. Matini tatu hizo zinatofautiana hapa na pale, na hili halishangazi. Inaonekana waandishi walionakili mazungumzo ya Mwalimu walifanya uamuzi juu ya masuala ya alama za maandishi, maneno yaliyokuwa yanajirudia, matumizi ya maneno yasiyokuwa sanifu, kutafsiri maneno ya Kiingereza na kadhalika. Sisi tumeamua kutumia ile matini tuliyoipata Butiama, kwa sababu ndiyo pekee haiku "safishwa". Inasomeka kama matini ya kunena na siyo ya kuandikwa, yaani, inasomeka kama mazungumzo halisi. Tunapenda kufikiri pia kuwa labda hiindiyo matini ambayo Mwalimu mwenyewe aliihitari, ndiyo maana ikaweko Butiama.

Dhana ya kazi ni msingi mojawapo muhimu katika maongezi (discourse) ya wajamaa. Na sio tu wajamaa lakini pia wanasiasa-uchumi (political economists) wa karne ya 18 na 19 huko Ulaya, wakiwemo Adam Smith, David Ricardo na, bila shaka, waasisi wa Ujamaa wa Kisayansi, Karl Marx na mwenzake Frederick Engels.* Tunapozungumzia kazi hatuna budi kutofautisha sura mbili za dhana hii – sura yake ya kifalsafa na sura yake ya siasa-uchumi. Katika mazungumzo yake na wanastudy-group, Mwalimu ameegemea zaidi kwa upande wa falsafa ya kazi kuliko siasa-uchumi yake. Kwa jumla, kwa maoni yangu, Mwalimu alipenda zaidi na pia kuelewa zaidi masuala na hoja za kifalsafa (na za kisiasa) kuliko zile za siasa-uchumi. Uelewa wake wa siasa-uchumi ulikuwa wa wastani, ukijikita zaidi kwenye siasa-uchumi ya akina Adam Smith kuliko ya akina Marx. Nimegusia tu jambo hili ambalo labda linahitaji kufanyiwa utafiti zaidi. Basi turudi kwenye 'soga' la Mwalimu.

Mtindo anaotumia Mwalimu katika 'soga' hili ni ule wa mazungumzo, sio hotuba. Hata hivyo Mwalimu alikuwa na kipaji kikubwa katika kupanga

---

*Hoja kwamba chanzo cha thamani ya kitu ni kazi ya binadamu ni kutoka enzi za zamani hata kabla ya karne ya 18. Mwanazuoni maarufu wa Kiarabu, Ibn Khaldun (1332-1406), alitoa hoja hiyo karne ya 14.

mazungumzo yake, lengo likiwa kumchemsha bongo msikilizaji bila ya kumchosha– yaani, kama alivyokuwa anasema bi mkubwa mmoja, mazungumzo mazito pamoja na masihara humohumo.

'Kazi ni uhai', Mwalimu anarudiarudia kusisitiza. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba bila kazi mwanadamu haishi; mwanadamu ni mwanadamu kwa sababu kazi ndio inadhihirisha, ni dalili ya, ubinadamu wake. 'Ubinadamu na kazi havitengwi.' Kazi ndio kiungo kati ya binadamu na mazingira yake, mazingira-asili pamoja na mazingira-jamii. Kwa hivyo, Mwalimu anahitimisha, kazi ni jambo la fahari kwa binadamu. Kama ni hivyo ilivyo, kwa nini tunakuta katika jamii tunamoishi, kazi inachukuliwa kama bughdha, kitu cha kulazimika kufanywa,'kitu cha dharau dharau', badala ya kitu cha kufurahia. Jibu lake ni muundo wa kazi katika mfumo wa kibepari.

Katika mfumo huu wa kibepari mfanyakazi anafanyishwa kazi kumfaidisha bepari. Kwa hivyo, anafanya kazi kwa ajili ya kuishi yeye mwenyewe na anafanyishwa kazi ya ziada na bepari ili kundi hili la wasiofanya kazi sio tu waishi bali wajilimbikizie mali – kwa maana ya kazi-mfu. Kwa hivyo, uhai wa ubepari hutegemea kazi. Wachache huishi bila kufanya kazi na wengi huishi kwa jasho lao la kazi – yaani kuna matabaka mawili yanayoainisha mfumo wa kibepari – wavujajasho na wavunajasho.

Mwalimu hatumii misemo ya kazi-hai (live labour) na kazi-mfu (dead labour) ambazo ni dhana za siasa-uchumi lakini mfano anaoutoa wa wamiliki wa mashoka, unaashiria dhana hizi. Shoka ni zana ya kufanyia kazi, anasema Mwalimu. Sasa kama wewe huna shoka na mwenzako analo, unaazima kufanyia kazi. "Ananiazima shoka nikafanyie kazi kwani inajulikana shoka ni kitu anachotumia binadamu kufanyia kazi. Mabepari wamegeuza hii kwani mashoka yanaazima watu – (kicheko) kwani badala ya watu kuazima mashoka yao yanaazima watu kwani yamekaa pale pale." Shoka lenyewe ni tunda la kazi, limetengenezwa na kuchongwa kwa kazi ya binadamu. Ni chombo kilicho na kazi ya mwanadamu, ni kazi-mfu, ambayo tunaiita *capital* au mtaji. Sasa kazi-mfu ndio inatumika na mmiliki wake kuwafanyisha kazi

wafanyakazi, yaani kazi-mfu inaifanyisha kazi kazi-hai! Mwenye kazi-mfu, shoka, ni bepari; mwenye kazi-hai, ni mfanyakazi. Mfumo huo ndio unavunja heshima na fahari ya kazi.

**Kuishi pamoja**

Insha hii ya mwisho bila shaka iliandikwa baada ya *Azimio la Arusha* na *Ujamaa Vijijini* kuelezea kiini na faida ya kuishi na kufanya kazi pamoja. Imeandikwa kwa lugha nyepesi isipokuwa hoja zake ni za kifalsafa inayosisitiza kwamba binadamu huishi na wenzake katika kundi la watu; hata kuzaa unahitaji binadamu mwenzako. Kwa hivyo, kuishi pamoja na kufanya kazi pamoja sio jambo geni bali katika mfumo wa kibepari – na mifumo mingine ya kinyonyaji – mtu mmoja, bepari, anafanyisha kazi kundi lingine kwa faida yake. Wafanyakazi wanafanya kazi pamoja lakini kwa kupangwa, kudhibitiwa, na kuamrishwa na bepari na matunda yao ya kufanya kazi kwa pamoja sio mali yao bali ni mali ya mwingine, asiyefanya kazi bali anayefanyisha kazi.

Nawaachia wasomaji wenyewe wasome insha hizi na kuonja utamu wake, sio tu ujumbe uliyomo ambao ni wa msingi kabisa, lakini pia mitindo yake, msamiati uliyotumika na ladha yake. Ukiweza kufananisha na chakula, insha hizi ni chakula cha kulamba polepole sio cha kuvamia mara moja; kadri unavyoramba, ndivyo unatamani kisiishe ili uendelee kuramba.

# 1

## Watu Wote ni Sawa?

Nilipokuwa mtoto nilipata kuambiwa hadith ambayo pengine hata wewe umepata kusikia au kuambiwa; ni hadith ya vipofu wawili waliokwenda porini kumtazama tembo. Wa kwanza "alimtazama" tembo kwa kuupapasa mkonga wake; bali yule wa pili alifanya utafiti wake kwa kulipapasa sikio. Walipokuwa wakirudi nyumbani walianza kubishana maana kipofu wa kwanza (kama kwamba yeye peke yake ndiye kamwona tembo) alimwambia mwenzake kwamba tembo ni kama kono refu na nene. Kipofu wa pili hakukubali, akasema, "Umedanganyika mwenzangu; tembo si kama kono refu na nene; tembo afanana na ngozi kubwa na pana."

Kila mara nijiulizapo, Je, watu wote ni sawa? Naikumbuka hadith hii ya utoto wangu. Najua kuwa mtu akisimama mbele ya umati wa watu, tuseme sokoni, na kusema, "Sikilizeni, enyi wauzaji na wanunuzi, watu wote ni sawa; kwa hiyo haifai kumwuzia mnunuzi huyu ndizi nyingi zaidi kuliko umwuziazo mnunuzi yule, wala kununua kwa muuzaji huyu nyanya nyingi zaidi kuliko ulizonunua kwa mwuzaji yule", wale watu wanaomsikiliza watafadhaika akilini mwao. Wao pia wana mnong'ono mioyoni mwao, mnong'ono ambao ni vigumu kuunyamazisha uwaambiao kwamba watu wote ni sawa. Lakini wakiangaza macho yao umatini mioyo yao inapagawa mashaka. Hapa wanamwona Shabani ambaye yu tayari kununua nyanya moja kwa senti nane; pale kuna Hassani na Thomas ambao si siku nyingi tangu walipopata adhabu kwa uhuni na unyang'anyi; pale kuna Rajabu, nguo zake maridadi na wala hana makuu; huyu hapa.

Binti Juma, mshairi maalum na wala hakwenda shule; na yule pale ni binti Pita ni mwalimu wa shuleni hajui guni ni nini, wala havijui vina. Je, watu hawa na wengine wote waliomo umatini humu ni sawa?

**Watu si Sawa katika Vipawa vyao**

Kwa maana moja watu wote ni sawa kabisa; yaani kila mtu ni sawa kabisa na mtu mwingine hamzidi wala hapungui; na kwa maana nyingine wote si sawa; yaani hakuna watu wawili mahali popote duniani ambao ni sawa bila mmoja kumzidi mwenzake katika jambo fulani. Kwanza tutazame ni katika maana gani ambayo watu wote si sawa.

Nikiingia katika kiwanda wanamo tengeneza mapesa, naweza kuomba nikaonyeshwe sarafu mbili mpya, tuseme sarafu za shilingi moja, ambazo ni sawasawa kabisa kwa kila hali. Sarafu moja ni sawa na nyingine kwa upya, upana, uzito, thamani, umbo, alama na kila kitu. Naweza kuonyeshwa mfuko au sanduku lenye maelfu ya sarafu zifananazo hivyo; naweza kufumba macho na kuingiza mkono katika mfuko au sanduku hilo na kutoa sarafu moja moja, na kila sarafu nitakayoitoa ni sawasawa kabisa na sarafu nyingine. Kufanana kwa namna hii ndiko kunakotufanya tuseme, 'Kulwa na Doto wanafanana kama mapesa.' Tu katika kuthibitisha jinsi mapacha wawili wanavyofanana. Kumbuka lakini nimelinganisha sarafu mpya. Nimefanya hivyo kwa sababu mara ukianza kulinganisha sarafu mpya na kuukuu unajua mara moja kwamba unalinganisha vitu viwili ambavyo si sawa. Moja labda ndiyo mara itoke kiwandani na kama ni yako hupendi hata kutumia kwa kumnunulia mkeo sukari; nyingine labda ilitoka kiwandani zamani za miaka ishirini, imelika ni chafu huipendi. Ni wazi kwamba hata sarafu, ingawa ni sawa sheriani, ingawa ni sawa katika thamani, ingawa zaweza kuwa sawa kwa kila hali, kwa desturi sarafu zote si sawa.

Lakini Binadamu hawawezi kuwa sawa kama sarafu zile mpya tulizozifananisha. Huwezi kupata binadamu wawili wenye sura moja, uzito ule ule, urefu ule ule, walao chakula kile kile; wenye nguvu sawa, mali sawa; afya sawa, marafiki sawa, maadui sawa; watakaoishi miaka ile ile, na kufa siku ile ile, wakati ule ule, kwa kisa kilekile. Ukiwapata Binadamu wa namna hiyo utakuwa umegundua wanyama wageni si Binadamu, na mimi kwa upande wangu nitakuwa na mashaka kama wanyama wenyewe ni viumbe kama viumbe wengine. Maana inaelekea kuwa sharti moja la

viumbe wote, hasa viumbe wenye nafsi, ni kuhitilafiana, na kuhitilafiana ni kutokuwa sawa. Ukikuta 'Binadamu' wawili ambao ni sawasawa kabisa kwa kila hali, yaani Binadamu 'A' ni sawasawa kabisa na Binadamu 'B', basi 'A' na 'B' si Binadamu wawili, bali ni nafsi mbili za mtu yule yule. AB ni mtu mmoja mwenye nafsi mbili; na hilo ni jambo lisilowezekana kwa kiumbe yeyote. Ni sharti la kuwa kiumbe kwamba kila kiumbe awe yeye asiwe kiumbe mwingine, na kwamba kila kiumbe awe tofauti asiwe sawa na kiumbe mwingine.

Hili ni jambo ambalo ni dhahiri lakini haliondoi ule mnong'ono tuusikiao moyoni kwamba watu wote ni sawa, na katika hadithi ya Binadamu kuna nyakati ambapo mnong'ono huo umekuwa kelele iliyonyamazisha kila kitu. Kwa mfano katika Karne ya kumi na nane Waamerika walipokuwa wakipigana na Waingereza ili kujipatia uhuru wao waliandika maneno haya katika Taarifa yao ya uhuru.

> Twaamini Kanuni hizi kuwa ni dhahiri: kwamba watu wote wameumbwa sawa, na kwamba wamepewana muumba wao haki fulani ambazo hawawezi kunyang'anywana kwamba baadhi ya haki hizi ni Uhai,Uhuru na Kutafuta Furaha.

Katika karne hiyo hiyo Wafaransa nao walifanya maasi makuu wakauwa watu wengi ajabu. Kisa? "Uhuru! Usawa! Udugu!" Walichinja watawala wao na kuanzisha dola mpya ambamo ilitazamiwa kuwa watu wote watakuwa sawa. Warusi hawakukubali kuachwa nyuma; wao pia katika karne hii wamechinja watawala wao ili kuanzisha dola ambamo watu wote watakuwa sawa. Lakini katika jambo lililokuwa wazi kabisa ni hili, kwamba watu wote si sawa. Kisa cha ugomvi wa Waamerika ni kwamba mfalme George III na washauri wake walipenda Waamerika kutoka London, kama vile warithi wao wanavyotawala Wakikuyu na Waganda siku hizi. Hili halikuwapendeza Waamerika ambao walikataa kutawaliwa kutoka London, wakisema kwamba wao si watoto, ni watu wazima sawasawa na Waingereza, na kwamba maadamu Waingereza wanajitawala na kuongoza mambo yao wao wenyewe

basi wao pia, Waamerika, ni budi wajitawale na kuongoza mambo yao wao wenyewe. Kisa cha ugomvi wao kilikuwa ni swali hili hili tunalojaribu kujibu sasa: Je, watu wote ni sawa? Hawakukubaliana katika majibu yao, wakagombana.

Mwisho wake ulikuwa nini? Waingereza walipigwa wakawaachia Waamerika wajitawale wenyewe. Hatuwezi kusema kwamba hii ilionyesha kuwa Waamerika ni bora au ni mashujaa zaidi kuliko Waingereza, lakini ni dhahiri kwamba haikuhakikisha kwamba watu wote ni sawa. Kusema kweli kama Waamerika wangeamini tangu mwanzo kwamba watu wote ni sawa lingekuwa ni jambo la hekima kwao kutii kinyonge na kukubali watawaliwe na Waingereza. Kwa nini? Kwa sababu wao walikuwa ni wachache zaidi kuliko Waingereza, walikuwa hawana jeshi, hawana utajiri kama wa Waingereza na wala hawana umoja. Basi kama ingekuwa ni kweli kwamba kila Mwamerika ni sawasawa kabisa na kila Mwingereza kama sarafu na sarafu, ni wazi kwamba Waamerika wangepigwa na Waingereza kama watoto, na kwamba ingekuwa ni wazimu kwa Waamerika wachache kuanzisha vita na Waingereza wengi na kutumaini kuwa watashinda. Kwa sababu Waamerika walikuwa na upungufu wa watu, na mali na majeshi, ilikuwa lazima waamini kwamba wana vipaji fulani ambavyo Waingereza hawana, au hawana kwa wingi kama wao, na ambavyo vitawawezesha kushinda.

Siwezi kuamini kwamba Bwana Thomas Jefferson alipoandika maneno hayo niliyoyatafsiri hapo juu aliamini, na wala sikubali kwamba akina Yankee wanataka tuamini, kwamba kila M-yankee ni sawa na Jefferson katika madaha, ufasaha na akili na kila askari wao ni sawa na George Washington katika ushujaa, uaminifu na huruma. Siwezi kuamini kwamba Wafaransa waliopiga kelele “Uhuru! Usawa! Udugu!” waliamini, au walitaka tuamini, kwamba kila Mfaransa ni sawa na Robespierre katika majivuno, akili na kupendwa; au kila raia ni sawa na Napoleon katika ujasiri, maadili na haki. Wala haiwezekani kwamba Warusi waliamini kwamba Warusi wote ni sawa, kwamba Warusi Weupe na Warusi Wekundu ni sawa, kwamba Nicholas III ni sawa na Lenin na Trotsky na Stalin. La, si dhahiri kwamba watu wote ni

sawa. Ili yale maneno ya Jefferson katika Taarifa ya Uhuru wa Waamerika yawe ya kweli kabisa ingefaa yaandikwe hivi:

> Twaamini Kanuni hizi kuwa ni dhahiri: kwamba ingawa watu wote si sawa wamepewa na Muumba wao haki fulani ambazo hawawezi kunyang'anywa, na kwamba baadhi ya haki hizi ni Uhai, Uhuru na Kutafuta Furaha.

Bila kufanya hivyo ule mnong'ono wa usawa wa Binadamu unaweza kutusahaulisha ukweli ulio dhahiri zaidi kwamba Binadamu wote si sawa.

Nimelitilia mkazo jambo hili kwa sababu mbili. Kwanza, kuna watu wasiopenda kuambiwa kuwa Binadamu si sawa.

Watu hawa wanafikiri kuwa ubora wa Binadamu unategemea usawa wao; na kwamba kama Binadamu wote si sawa, hawafai; kwamba siku hiyo itakuwa siku ya maafa makubwa kwa Binadamu itakapohakikishwa kwamba watu wote si sawa. Hofu hii ni hofu ya maana kabisa lakini usawa wanaoufikiri ni usawa ambao haupo na wala si usawa unaotamanika. Kwa upande wangu naamini kwamba siku hiyo italeta maafa makubwa kwa Binadamu watu wote wataposawazishwa kama sarafu. Binadamu ni sawa kwa maana ambayo tutachungua baadaye lakini binadamu hawapendi kuwa sawa kama mapesa. Wewe unaweza kunizidi akili, mali, nguvu, uzuri wa umbo, wema, upole na kila jambo. Lakini ingewezekana Mwinyezi Mungu aniulize kama nitapenda anipe karama alizokupa kwa kunifanya wewe ningekataa maana ingawa sipendi unyonge wangu napenda kuwa mimi. Nikipewa karama zako zote kwa kufanywa wewe wa pili sikupewa kitu, nimefutwa katika viumbe vya Mungu. Hilo ni afa kubwa zaidi kuliko unyonge wangu na afa lingine lolote liwezalo kunipata.

Pili, kuna watu wengine wanaotambua kwamba binadamu wote si sawa. Wao pia kama hao wa kwanza hawapendi kuhitilafiana huku kwa binadamu kwa hiyo wanataka binadamu wasawazishwe. Wewe na mimi twajua kwamba jambo lenyewe haliwezekani na halitamaniki, lakini wao wanalipenda sana.

Nadhani kwanza wangependa wenye nguvu wawateketeze wanyonge; kisha warefu wawateketeze wafupi, halafu wenye akili wawateketeze wajinga, baadaye wazuri wawateketeze wabaya, mwisho wazima wawateketeze wagonjwa, na kadhalika, sijui watakomea wapi.

Fikra za kipumbavu kama hizi ndizo zinazonikumbusha hadithi ile ya vipofu wawili waliokwenda porini kumtazama tembo. Binadamu wanahitilafiana; kutokuwa sawa ni kipaji cha Binadamu kama vile mkonga au sikio ni kiungo cha tembo.

Lakini kama vile mkonga au sikio si tembo mzima; kuhitilafiana si Binadamu mzima. Tunaelewa kwa nini vipofu waligombana. Jambo ambalo tukiambiwa hatuwezi kuelewa ni kwamba kina Binitembo wote wamegawanyika katika mafungu mawili, fungu moja likisema kwamba tembo wote ni kama wanene, na fungu lingine linakataa likiamini kwamba tembo wanafanana na ngozi kubwa na pana. Tungewasikia Binitembo wakiwa katika ubishi kama huu tungeangua vicheko; lakini labda tungewahurumia, maana akili za tembo ni za kitembo. Kichekesho kikubwa zaidi ni kwamba Binadamu wanafanya ubishi huu huu usio na maana. Kuna Binadamu ambao wamepapasa kuhitilafiana kwao na wanaamini kuwa watu wote si sawa; kuna wengine ambao wamepapasa usawa bila kupapasa kutofautiana, na wao wanaamini kabisa kwamba watu wote ni sawa. Sisi tumepapasa kutokuwa sawa kwa binadamu, hebu sasa natupapase usawa wao.

### Binadamu ni Sawa katika Ubinadamu

Binadamu wote ni sawa katika ubinadamu wao. Juma na Mwajuma hawahitilafiani katika ubinadamu wao. Katika mambo mengine yote Juma na Mwajuma si sawa, lakini katika ubinadamu wao hawahitilafiani hata chembe. Wewe huwezi, mimi siwezi, mtu mwingine yeyote hawezi, na wala Mwinyezi Mungu hawezi kumfanya Juma awe binadamu zaidi kuliko Mwajuma au kumfanya Mwajuma awe binadamu zaidi kuliko Juma. Mwinyezi Mungu aweza kufanya jambo ambalo wewe na mimi na wenzetu wengine hatuwezi

kufanya-anaweza kumuumbua Juma na anaweza kumfanya Mwajuma awe kiumbe mwingine bora au hafifu zaidi kuliko binadamu, lakini hawezi kumfanya Juma au Mwajuma awe binadamu bora au hafifu zaidi kuliko binadamu wengine, hawezi kuongeza wala kupunguza ubinadamu wao.

Jambo lenyewe lisikutishe bure, si gumu kuelewa. Tuchukue mfano. Labda ulipokuwa shule ulipata kuambiwa kuwa kuna namna fulani ya hewa iitwayo "oxygen" (na tuiite "O" kwa kifupi) na namna nyingine iitwayo "Hydrogen" (tuiite "H" kwa kifupi). Pengine uliambiwa pia kwamba hewa inaweza kupimwa au tuseme "kuhesabiwa" kama vile tupimavyo mchele katika vibaba au kuhesabu kondoo. Ikiwa ulipata bahati (au mkosi!) zaidi labda uliambiwa kwamba ukichukua vipimo viwili vya "Hydrogen" (tuviite $H_2$) na kuvichanganya namna fulani na kipimo kimoja cha "Oxygen" ($O_1$) utapata $H_2+O_1=H_2O_1$. Kitu hicho si "Hydrogen", si "Oxygen" na wala si hewa tena, ni kijitone cha maji haya haya unayokunywa na kuoga. Na maji yote duniani ni $H_2O$; ndiyo kusema kwamba maji yote duniani ni maji. Ni kweli kwamba kuna maji machafu na maji safi, maji matamu na maji ya chumvi, maji ya kisima na maji ya mvua, maji ya mto na maji baridi; ni kweli kwamba kwa kuyachuja haya, kuyaondoa chumvi, kuyapooza haya tutayapunguzia au kuyaondoa uchafu, chumvi au joto. Lakini hatuwezi kuyaongezea wala kuyapunguzia umaji wao, maana katika umaji wake maji yote ni sawa. Na si hivyo tu; katika umaji wao maji yote ni kamili na haiwezekani yaongezewe au yapunguziwe umaji wao na yabaki kuwa maji. Tukisema kwamba hata Mwinyezi Mungu hawezi kuyaongezea wala kuyapunguzia umaji wao hatusemi kwamba hawezi kuyaumbua au kuyafanya kitu kingine, tunasema tu kwamba hawezi kuyapunguzia au kuyaongezea umaji wao na yaendelee tena kuwa maji. Mwinyezi Mungu hawezi kufanya jambo la upumbavu, na kuumba maji ambayo si maji; si upumbavu tu, ni jambo lisilowezekana.

Kadhalika, Mwinyezi Mungu hawezi kuumba binadamu ambaye si binadamu. Kiumbe aliye chini ya binadamu si binadamu na kiumbe aliye juu ya binadamu si binadamu. Katika ubinadamu wao binadamu wote ni sawa <u>tena ni kamili</u>.

Tukisema kuwa binadamu si kamili tunaweza kuwa na maana moja tu, kwamba binadamu si sawa na Mungu, na kwa maana hiyo hakuna kiumbe ambaye ni kamili, Mungu peke yake ndiye aliye kamili. Lakini ikiwa tusemapo kwamba binadamu si kamili nia yetu ni kusema kwamba Mwinyezi Mungu angeweza kuumba binadamu aliye kamili zaidi kuliko binadamu tunasema jambo la upumbavu. Kiumbe huyo asingekuwa binadamu angekuwa ni kiumbe mwingine kabisa.

Mfalme na raia wake, jemedari wa majeshi na askari wake, nahodha wa manowari na mabaharia wake, malkia na wajakazi wake, hakimu na washtakiwa, bawabu na mfungwa, daktari na mgonjwa, mwalimu na mwanafunzi, wazima na vilema, werevu na wajinga, wenye akili kamili na wendawazimu, watakatifu na wenye dhambi, wenye dini na washenzi, mzazi na mwanae, waliozaliwa na walio tumboni; wote hawa ni binadamu kamili na sawasawa katika ubinadamu wao.

Usawa huu wa watu wote katika ubinadamu wao na tofauti ya watu katika vipaji vyao ni mambo dhahiri na wala hayapingani. Kuwasawazisha binadamu katika vipaji vyao si jambo linalotamanika maana ni kuwafuta na kuacha binadamu mmoja mwenye nafsi malaki; na kuwahitilafishana binadamu katika ubinadamu wao pia ni jambo lisilotamanika, maana pia ni kuwafuta: ni sawa na kuwa na ulimwengu wenye mtu mmoja, kuku mmoja, nyoka mmoja, ng'ombe mmoja na kadhalika. Uzuri wote tunaoujua wa kuishi na kupendana na kusaidiana na binadamu wenzetu utaondoka.

## Binadamu ni Sawa na Tofauti katika Nafsi

Nasema, kuwa sawa na kutokuwa sawa huko ambako nimekueleza ni mambo yaliyo dhahiri; lakini kuna usawa na kutokuwa na usawa kwa namna nyingine ambako si dhahiri hivyo. Nitajaribu kukueleza kwa kuchukua mfano wa sarafu tena. Sarafu, kama vile binadamu, zinaweza kuhitilafiana katika mambo ya uzito na mng'ao. Tulisema pia kwamba, ingawa sarafu zinaweza kuhitilafiana, yawezekana kupata sarafu mbili au zaidi ambazo ni

sawasawa kwa kila hali. Jambo moja ambalo hatukusema ni kwamba sarafu mbili kama zikihitilafiana au zisihitilafiane zote mbili, ikiwa zinakubaliwa na Serikali, zina thamani ile ile. Kama ukinikopesha sarafu ya shilingi moja unatazamia kwamba nitakulipa kwa sarafu nyingine ya shilingi, lakini siyo kwamba nitakurudishia sarafu ile ile uliyonikopesha. Kwa kweli haki si lazima nikurudishie shilingi nyeupe; mashtaka wewe ni ile thamani ya shilingi moja na ninaweza kukurudishia thamani hii kwa kukupa senti mia, sarafu mbili za senti hamsini, noti ya shilingi moja au hata noti ya shilingi kumi ili mradi unirudishie shilingi zangu tisa. Jambo kubwa hapa, nasema, ni ile thamani, na mbele ya sheria shilingi zote zinazokubaliwa zina thamani ile ile hata kama nyingine ni fedha, zingine za karatasi na zingine ni kifuko cha sarafu za shaba. Kwa maana hii ya thamani mbele ya sheria tunaweza kusema kwamba katika ushilingi wao shilingi zote ni sawa. Lakini usawa huu wa shilingi ni tofauti sana sana na usawa wa binadamu.

Mzee akiniletea mtoto wake shuleni kwangu anatazamia kuwa wakati wa mapumziko nitamrudishia mtoto wake yule yule. Hawezi kukubali kupokea mtoto mwingine badala yake hata kama kwa vipimo vyote vya duniani mtoto huyo ni mtoto bora katika kila kipaji kuliko mtoto wake mwenyewe. Ni kweli kwamba watoto hao hawahitilafiani katika ubinadamu wao; lakini kuna kitu fulani juu yao ambacho kinafanya isiwezekane kabisa kubadilishana. Kitu hiki hata sijui nikipe jina [ ]* kutudanganya.

Mfuga watumwa anaweza kukubali arudishiwe mtumwa mwingine badala ya mtumwa wake; kwa sababu anachotaka ni kile ulichotaka uliponikopesha shilingi; anataka thamani. Kwa ajili hiyo atafurahi sana akirudishiwa mtumwa mwenye akili, afya, nguvu na utii zaidi kuliko mtumwa wake mwenyewe. Kadhalika nikiandika barua kwa Bwana Mwalimu kumwomba kazi anachotaka ni ile thamani yangu inayonifanya kuwa mwalimu siyo thamani inayonifanya kuwa mimi; kwa kuangalia ile thamani inayonifanya kuwa mwalimu anaweza kunikubali au kunikataa na kuchagua mwalimu mwingine; lakini akijali ile thamani inayonifanya mimi hana budi anikubali,

* Mabano ya aina hii yanaashiria kukosekana kwa maneno fulani, ama kwa sababu hayasomeki kwenye matini-asili, au hayaonekani kabisa.

kwa sababu hakuna mimi mwingine duniani, kwa hiyo hawezi kupokea mtu mwingine badala yangu. Kwa kukosa jina zuri zaidi nitakiita kitu hiki thamani ya nafsi. Kwa thamani ya nafsi, yangu mimi ni tofauti kabisa na binadamu wengine; ndicho kitu peke yake ambacho hatushirikiani na binadamu mwingine yeyote. Thamani ya nafsi ni thamani ya pekee; ndiyo thamani inayomfanya kila binadamu awe yeye asiwe binadamu mwingine. Vitu vingine vyote, utu, akili, ujinga, ufupi, urefu, mawazo, tamaa na kadhalika binadamu wote wanashirikiana. Ni kama kwamba binadamu wote walivichota katika kisima kile kile; katika kisima cha ubinadamu wote walipewa vyombo sawasawa wakachota ubinadamu sawasawa; katika visima vya vipaji kila binadamu alipewa chombo ambacho ni tofauti na cha mwenzake lakini kwa kila kipaji wote walichota katika kisima kile kile; lakini katika kuchota nafsi kila binadamu alipewa chombo ambacho ni sawasawa kabisa na cha mwenzake lakini kila mtu alipewa kisima cha pekee.

Jambo linalofanya isiwezekane kubadilishana binadamu ni hili; kwamba vitu visivyo sawa haviwezi kulinganishwa.

Sasa utaona kwa nini nilisema kwamba kuhitilafiana huku ni jambo gumu zaidi kueleza kuliko kule kuhitilafiana kwa vipaji. Huku ni kuhitilafiana ambako kunawafanya binadamu wawe sawa kwa maana kubwa zaidi kuliko ile maana ya kuwa sawa katika ubinadamu wao. Tunaposema kuwa mbele ya Mungu watu wote ni sawa sina shaka tuna maana kubwa zaidi kuliko maana ya usawa wa ubinadamu; maana usawa huo ni usawa unaohusu viumbe vingine pia. Kondoo wote ni sawa katika ukondoo wao, kunguni wote ni sawa katika ukunguni wao; na mbele ya Mungu, au kiumbe aelewaye jambo hili, kondoo wote ni sawa na kunguni wote ni sawa. Lakini kondoo hana nafsi na wala kunguni hana nafsi. Kondoo ni mnyama katika kundi na kunguni ni mdudu katika kundi. Kondoo hajijui, na hana "umimi" juu yake; kadhalika kunguni hajijui na hana ''umimi'' juu yake. Lakini binadamu ni tofauti. Kile kinachomfanya awe sawa na wengine mbele ya Mungu siyo kile kinachomfanya awe mmoja katika kundi; yaani ubinadamu wake, ni kile kinachomfanya yeye, yaani thamani ya nafsi yake, na hiki hashirikiani na

mtu mwingine, ni kitu chake pekee. Katika sura ya pili ya Ufunuo kifungu cha 17 kuna maneno haya:

> Aliye na sikio na asikie yale ambayo Roho ayaambia makanisa: Kwa yule atakayeshinda nitampa mkate uliofichwa; na nitampa kinga nyeupe, na katika kinga hiyo litaandikwa jina jipya ambalo hakuna mtu alijuaye isipokuwa yule alipewaye.

Jina jipya hili ni nini, kama si nafsi? Ndilo jina la pekee ambalo alijua yule tu aliyepewa. Sasa hata sisi wenyewe hatulijui jina hilo barabara, lakini itakapompendeza Mwinyezi Mungu kutufunulia kila mmoja wetu atalijua jina lake kama vile mtu mwingine atakayelijua hivyo.

## Mataifa yote ni Sawa?

Ukiniuliza kama mataifa yote ni sawa jibu langu litategemea unavyofikiria. Ikiwa, kwa mfano, unapenda kujua kama wazungu na [ ] sawa kwa wingi jibu ni la; wazungu ni wengi zaidi kuliko [ ]. Na kuhitilafiana huku kwa wingi kunadhihirisha mambo mengine mengi. [Ikiwa] mataifa mawili si sawa kwa wingi basi ni upumbavu kufikiri kuwa mataifa yote yatakuwa na hesabu ile ile ya watu warefu, wafupi, werevu, wajinga, matajiri, maskini, watakatifu, waovu, na kadhalika. Sheria zote tunazojua za hesabu zinafanya usawa wa namna hii usiwezekane.

Vile vile ikiwa unapenda kujua kama Waafrika wowote wawili, kwa mfano, ni sawasawa kabisa na Wahindi wowote wawili kwa uzito, urefu, akili na kadhalika, jibu langu ni la. Kwa sababu watu wawili ni Waafrika na wengine wawili ni Wahindi tunatazamia kwamba watakuwa tofauti zaidi kuliko kama wote wanne wangekuwa ni Waafrika au Wahindi. Ukiigawanya nchi yoyote katika sehemu mbili watu wa sehemu moja na sehemu nyingine watakuwa karibu sawa kwa vipaji fulani fulani, na watahitilafiana sana kwa vipaji vingine. Usawa wao utategemea jinsi vipaji hivi vilivyokuwa vimetapakazwa nchini kabla haijagawanywa katika sehemu mbili. Lakini hata ukijitahidije kuvisawazisha vipaji vyenyewe sehemu zile mbili haziwezi

kulingana, maana ni sehemu za nchi wanamoishi binadamu si mifuko ya ngozi zilimowekwa sarafu.

Ikiwa hiyo ni kweli juu ya sehemu mbili za nchi ili ile wanamoishi watu wa taifa lile lile sembuse nchi mbili mbali mbali wanamoishi watu wa mataifa mawili mbalimbali; mataifa ambayo yametengwa na maelfu ya maili za maji au nchi kavu, maelfu ya miaka ya historia mbali mbali, hali ya nchi tofauti, lugha tofuati, mawazo tofauti, mila tofauti, na mambo mengine kadha wa kadha. Kwa upande wangu ni jambo lililo dhahiri kabisa kwamba kama vile hakuna binadamu wawili ambao ni sawa, kadhalika hakuna mataifa mawili ambayo ni sawa. Ukiyagundua mataifa mawili ya namna hiyo tambua mara moja kwamba si mataifa mawili mbali mbali bali ni mafungu mawili ya taifa lile lile.

Lakini kuhitilafiana kwa mataifa ni tofauti na kuhitilafiana kwa watu wawili. Kama nilivyokwisha kusema taifa la watu si mfuko wa sarafu, ni jamii ya binadamu ambao hawalingani katika hali yoyote isipokuwa ubinadamu wao. Tukisema kwamba senti za Kiamerika ni bora zaidi kuliko senti za Afrika ya Mashariki maana yetu ni kwamba senti yoyote ya Kiamerika ina thamani kubwa zaidi na kwamba inaweza kununua bidhaa nyingi zaidi mahali popote duniani kuliko senti yoyote ya Afrika ya Mashariki. Kwa maana hii kila senti ya Kiamerika ni bora zaidi kuliko senti yoyote ya Afrika Mashariki. Na hii inawezekana kwa sababu senti zote za Kiamerika zina thamani ile ile na senti zote za Afrika ya Mashariki zina thamani ile ile. Kama isingalikuwa hivyo basi ingalikuwa lazima kuifanya senti hafifu zaidi kuliko zote za Kiamerika iwe bora zaidi kuliko senti yenye thamani kubwa zaidi kuliko zote za Afrika ya Mashariki.

Lakini kwa binadamu tunajua kwamba sharti la kwanza haliwezekani. Waamerika wote si sawa katika jambo lolote isipokuwa ubinadamu wao na kwa ubinadamu wao hawahitilafiani na binadamu wengine. Sharti la pili pia haliwezekani, ingawa karibuni hivi nilisoma barua ya mwanamke mmoja mzungu wa Northern Rhodesia anayeamini kwamba Mzungu mpumbavu kupita wote ni mwenye akili zaidi kuliko Mwafrika mwenye akili zaidi


kupita wote. Nasema jambo lenyewe haliwezekani na ni wapumbavu tu wanaodhani kuwa linawezekana [ ] la, hasha! Nitajisahihisha. Siyo Wapumbavu tu wanaodhani kwamba ubora huu wa taifa moja kupita taifa lingine unawezekana. Hitler hakuwa mpumbavu, na Dr. Malau si mpumbavu na si wao tu wanaoliamini, nyuma yao kuna maelfu ya wafuasi. Mwaka 1933 wataalamu wa Kijerumani walikutana katika mji wa Nuremberg kuzungumza jambo hili na baada ya kubarizi kwa busara na hekima walikubaliana na kutoa taarifa yenye maneno haya: "Kati ya mataifa yetu bora na viumbe hafifu ambavyo bado vinaitwa binadamu kuna tofauti kubwa zaidi kuliko tofauti iliyoko kati ya mtu wa chini kabisa na nyani wa juu kupita wote." Ndiyo kusema kwamba wataalamu hawa, ambao hawakuwa watu wapumbavu hata kidogo, waliamini kwamba kati ya Wazungu na Waafrika (ambao ni kosa kuwaita binadamu) kuna tofauti kubwa zaidi kuliko ile iliyoko kati ya Mzungu mpumbavu na nyani mwerevu. Jambo lenyewe ingawa limesemwa na wataalamu linachekesha kidogo maana ikiwa ni la kweli basi Mzungu na nyani wamekaribiana zaidi kuliko Mwafrika na Mzungu na ni ajabu kumsikia mtu mwenye akili kama Hitler akiwaita Waafrika nusu nyani. Itawezekanaje? Maana kati ya Mwafrika na nyani kuna Mzungu! Au tuseme kati ya Mwafrika na Mzungu kuna nyani, na Mzungu na nyani wamekaribiana zaidi kuliko Mwafrika na nyani! Mwerevu akipumbazika humpita hata juha!

Jambo lenyewe lifikiri kwa namna nyingine. Nimeambiwa na wataalamu wa elimu ya viumbe kwamba huwezi kumtumia mnyama kama kondoo kuzalishia mbuzi kwa sababu wanyama wenyewe ni tofauti mno. Kadhalika huwezi kumtumia jogoo la kuku kuzalishia njiwa. Lakini hatuna haja kuambiwa na wataalamu wa elimu ya viumbe kutambua kwamba Mzungu (hata mwenye akili) na Mwafrika (hata mpumbavu kupita wote) watazaa watoto. Sasa basi, [tofauti] iliyopo kati ya Mzungu mpumbavu na nyani mwerevu ni ndogo zaidi [kuliko] iliyopo kati ya Mzungu yeyote na Mwafrika yeyote [ ] machotara wachache zaidi kati ya Wazungu na Waafrika kuliko kati ya [ ] na manyani.

Tuliache jambo lenyewe, ni la kipumbavu mno.

Watu wengi wanaoamini kwamba mataifa fulani ni bora kuliko mengine [ ] ni kwamba mpumbavu wa taifa bora ni mwerevu zaidi kuliko mwerevu wa taifa duni. Budi kuwe na ubora mwingine wanaoufikiri. Kwa mfano, je haiwezekani Mzungu mwenye akili kupita wote awe ni mwenye akili zaidi kuliko Mwafrika au Mhindi mwenye akili kupita wote? Kwa upande wangu naamini kwamba inawezekana sana. Katika kipindi chochote cha maisha ya binadamu inawezekana kabisa mtu aliye na akili zaidi au nzuri zaidi kupita wengine wote wa taifa lake pia awazidi werevu au wazuri wengine wote wa mataifa mengine. Na hii inawezekana kwa sababu hakuna watu wawili wowote mahali popote duniani ambao wana akili ile ile au uzuri ule ule.

Swali ambalo ni gumu zaidi ni hili, na ndilo liwasumbualo jamaa wengi: Je ikiwa mwaka 1952 binadamu mwenye akili kupita wote alikuwa ni Mhindi, ni kweli kusema kwamba miaka yote iliyopita binadamu mwenye akili kupita wote alikuwa ni Mhindi na miaka yote ifuatayo atakuwa Mhindi? Nadhani Wazungu wengi wanaoamini kwamba taifa lao ni bora kupita mataifa mengine wataandika "Mzungu" nilipoandika "Mhindi" na kujibu "ndiyo." Na nadhani pia Wazungu ambao baada ya kuandika "Mzungu" badala ya "Mhindi" watajibu "siyo" bila kusita ni wachache sana. Wazungu wengi, hata wale utakaowasikia wakisema kuwa watu wote tu sawa (ikiwa usawa waufikirio si usawa katika ubinadamu) wanaamini kwa mfano, kwamba ingawa Mwafrika mwerevu ni mwenye akili zaidi kuliko Mzungu mpumbamvu, kati ya werevu wawili, Mwafrika na Mzungu, Mzungu ni mwerevu zaidi kuliko Mwafrika. Wanaamini kwamba ukigawa Wazungu wote katika mafungu matatu kwa kadiri ya akili zao, Majitu, Wastani na Mbilikimo, na kuwagawa Waafrika wote vivyo hivyo, basi Majitu Wazungu watawazidi Majitu Waaafrika na Mbilikimo Wazungu watawazidi MbilikimoWaafrika, ingawa Majitu Waafrika watawazidi Wastani Wazungu na Wastani Waaafrika watawazidi Mbilikimo Wazungu.


Wazungu
Waafrika
Wazungu
Waafrika
Wazungu
Waafrika

# 2

## Kazi*

Waheshimiwa, nilipokuwa nakuja hapa nilifikiria nakuja kupiga soga tu, maana yake nitakuta kikundi kidogo hivi, halafu tutakaa tutapiga soga juu ya Azimio la Arusha na elimu tunayoihitaji katika nchi yetu ili kutekeleza siasa ya Azimio la Arusha. Sasa nafika nakuta ni umati mkubwa kabisa wa watu, sasa lazima nisimame kusema; na mtu hupigi soga huku umesimama (*makofi*). Soga hupigi mtu huku umesimama, wengine wamekaa wewe huku unapiga soga, sasa inakuwa natoa hotuba, na mimi sikuwa nakusudia kuja kutoa hotuba juu ya Azimio la Arusha. Lakini vyema, nitapiga soga huku nimesimama,lakini nitafanya soga, siyo hotuba.

Soga lenyewe ninalotaka kupiga ni juu ya kitu kazi, na kabla sijaanza hilo soga nataka kukuunga mkono Mheshimiwa mkuu wa kiti, sio kinara bwana, sisemi kinara (*kicheko*), Mheshimiwa mkuu wa kiti wa kikundi hiki cha TANU cha Mazungumzo kwamba  kikundi hiki kimeanzishwa kusudi tuzungumze siasa zetu. Kwa sababu sisi lazima tuitazame nchi yetu ilivyo, ilivyo nchi yetu na Afrika ilivyo, halafu tuseme kama hivyo ndivyo nchi yetu ilivyo, na kama hivi ndivyo Afrika ilivyo, na kama hivi ndivyo ulimwengu ulivyo, ni siasa gani zinazotufaa katika kuendesha majambo yetu. Lazima tufikiri; kazi ya kufikiri ni yetu wenyewe.

Na jambo moja ambalo viongozi wa TANU tunajitahidi kulieleza ni kwamba, hakuna msahafu. Hakuna msahafu wa mambo ya kuendesha nchi. Ujamaa si dini, hauna nabii, hatuna msahafu kama wa Kikristo una mitume wamekwisha amua, wamekwisha taja, wametumwa na Mungu, wakaja hapa wakatamka neno la Mungu,sasa kilichobaki kwetu sisi ni kujua Mungu kasemaje kwa kufuata vitabu vile, misahafu, na maana yake nini Mungu alivyosema.

* Mazungumzo ya Mwalimu Nyerere juu ya kazi kwa Tanu Study Group, 13 Juni 1967.

Au ni dini ya Kiislamu, ina msahafu wake na Mtume Mohammed. Sasa unasema "Mungu kasemaje", unafunua aya inayohusika, halafu unawauliza mashehe, "Mashehe hii aya maana yake nini?" Wakishakwambia basi, mambo yamekwisha huna haja ya kufikiri zaidi ya hapo!

Sisi tunakataa habari hii, juu ya Ujamaa. Juu ya Ujamaa tunakataa viongozi wa TANU. Tunasema hakuna msahafu wa Ujamaa. Kuna viongozi wengi, watu wengi wamewaza, na mawazo yao yanaweza yakatusaidia. Basi, hakuna zaidi ya hapo. Na kwamba sisi wenyewe hapa lazima tukae na kufikiri kwa kweli kweli. Kufikiri kwetu sio kufikiri kwa theology. Waliosomea theology wapo hapa akina Kasela Bantu (*kicheko*). Hawa wamesomea theology, hawa yaliwashinda; walikuwa mateka, lakini katika theology, ni kazi ya theology ni tafsiri ya yaliyosemwa na mitume; hakuna zaidi ya hapo, ni kutafsiri waliyosema mitume.

Sisi tunasema, viongozi wa TANU tunakuambieni, lazima mfikiri. Kufikiri kwenu ni kwa kweli kweli, ikiwezekana mkatupatia mawazo mapya, tupatie ya kutusaidia katika maisha yetu. Lakini kufikiri kwenu kusiwe ni kutafsiri waliyosema mitume, la, hakuna mitume katika siasa tunayoiwazia sisi. Hilo ndilo jambo kubwa na ndiyo maana tunawatakeni viongozi wa TANU mfikiri. Mkae na kufikiri. Mkae, mnakaa mnafikiri, unayatazama maisha yetu yalivyo, mnaitazama Afrika ilivyo, mnautazama ulimwengu ulivyo, mnafikiri ninyi wenyewe. Mkikuta kuna mtu alipata kusema jambo zamani, mkaona linatufaa, msikatae kulichukua, lazima muwe na mind open kabisa. Mkikuta kuna mtu ambaye kasema jambo ambalo linawafaa watu wengi lakini kwa hali yetu hivi sasa hivi ilivyo halitufai, likataeni. Msione ajabu kulikataa. Sisi tunataka kuwa watu free. Hatutaki kuwa watu hivi hivi tu. Hatutaki kuwa copyists, wala hatutaki kuwa watumwa, tukatae. Hatuwezi kukataa mawazo ya binadamu, hatuanzi civilization leo, civilization imeanza tangu zamani, mawazo ya binadamu yameanza tangu zamani, na yapo. Kwa hiyo, yanayotufaa chukua, yasiyotufaa tunayakataa. Lakini kitu tunachokataa number one ni msahafu katika kuendesha mambo yetu.

Hiyo ndiyo sababu ya kuanzisha kikundi hiki. Ni kwa matumaini kwamba

kweli tutapata vijana wetu watakaokaa na kufikiri. Lazima mfikiri, ndiyo kazi ya binadamu. Ni kufikiri na kufikiri na kufikiri. Kazi ya binadamu siyo kutafsiri maana za misahafu ya watu wengine. Siyo katika maisha haya; siyo katika maisha haya tunayosema ni ya Ujamaa. Ni sawa katika maisha ya dini, lakini hata katika maisha ya dini watu wana-question. Hiyo ndiyo sababu ya kuwepo kikundi hiki na ndiyo maana na mimi ninayo matumaini hayo hayo kama mliyonayo ninyi, tutaendelea na kitatusaidia katika kupanua mawazo.

Sasa nasema nimekuja mimi kuja kupiga soga. Nimekuja kupiga soga mwanzo huu wa semina yenu na soga lenyewe nataka kupiga juu ya kitu "kazi", Azimio la Arusha na kitu "kazi".

Katika Azimio la Arusha kitu kimoja kinatiliwa mkazo sana ni kujitegemea,kitu kinaitwa "kujitegemea". Ndicho kitu kikubwa katika Azimio la Arusha, kujitegemea. Kitu kingine kinatiliwa mkazo mle katika Azimio la Arusha ni mtu kupata riziki yake kwa kazi yake mwenyewe. Kuna watu wanaosamehewa mle katika Azimio la Arusha wanatajwa wale wanaosamehewa, watoto wadogo, vilema, wazee wasiojiweza; hapana mtu mwingine, mtu msamaha.

Kwa hiyo, mle kuna mkazo wa kujitegemea kwa mtu, kujitegemea mtu kwa nafsi yake, na kuna kujitegemea kwa nchi. Na kujitegemea kule tunasema ni "kazi". Sasa hakuna namna nyingine ya kujitegemea isipokuwa ni kazi; kwa hiyo, ndiyo maana nasema soga ninalotaka kulipiga mimi nataka kulipiga soga juu ya kitu "kazi".

Binadamu na kazi, na kitu kazi huwezi kuwatenga. Huwezi kutenga binadamu na kazi, kwamba unaufikiria ubinadamu na maendeleo, acha maendeleo, kuishi tu; acha habari ya maendeleo kwanza, kuishi tu, binadamu ana maisha, anakuwa, ana maisha halafu kitu kazi au shughuli hamna! Jitihada hamna! Ubinadamu na kazi havitengwi, huwezi kutenga binadamu na kazi.

Binadamu anakuja katika dunia hii ili kuishi; hana budi ashindane na matatizo fulani atakayoyakuta katika ulimwengu huu, lazima. Kuishi kwake kunataka

ale. Yeye si jiwe, jiwe ukilitupa likishaanguka hapo basi unalisahau. Lakini binadamu lazima ale, unamtupa katika ulimwengu huu - huu tunaoujuwa, sijui mwingine tena, sijui huko mbinguni au mahali - lakini huu tunaoujua, unamtupa hapa vuu, lazima ale.

Sasa atakulaje? Hakuna kula bila shughuli. Hakuwezekani, haiwezekani. Lazima kujimudumudu kutokee, hata kwa kitoto kidogo kile lazima kijimudumudu tu. Kama ni ziwa kinyonye, lazima. Kama kanashindwa kabisa tuna wasiwasi, kama kanashindwa kabisa katoto kale kunyonya, tukamiminie tu maziwa ndani. Lakini hata hivyo, lazima tutumaini katoto haka katajimudumudu, mwili wake lazima ufanye shughuli shughuli (*kicheko*). Lazima tutumainie kwamba angalau yakishaingia maziwa yakatumbukia ndani, kimwili cha mtoto huyu kitashughulika. Kisiposhughulika kitakufa, lazima kife.  Na ndiyo maana ya kufa.Maana ya kufa ni kwamba tukiukuta mwili huu umekaa, umepoa, haushughuliki tena, tunasema umekufa. Hauwezi tena kufanya kazi. Siyo kwamba hauwezi tena kufanya kazi, hamna kazi ndani, kazi imeondoka, uwezo wa kazi umeondoka, kazi hamna amekwisha. Tunaushika tunaona tunaukuta baridi, tunasema "huyu kafa". Ndiyo, amekufa. Mwili huu si active tena. Umekwisha kuacha kufanya kazi, ndipo tunaposema amekufa. Mwili umekwisha kuacha, ume-stop, umekoma kufanya kazi; ndiyo maana ya kufa. Kazi na maisha ni kitu kile kile, huwezi ukatoa tofauti ya kazi na maisha.

Sasa kazi na maendeleo. Kazi na maisha ni kitu kile kile. Mwili wa binadamu na binadamu mwenyewe anapoacha kufanya kazi, brain ikishaacha kufanya kazi, kesha. Limwili lake lazima liendelee kufanya kazi wakati wote, au sivyo ndio kesha, ndio maana ya kufa. Na maendeleo, acha habari ya maisha na kazi, lakini maendeleo na kazi ni kitu kile kile, hakuna namna nyingine sisi ya kuendelea, hatukupewa namna nyingine sisi ya kuendelea. Mungu yeye hataki maendeleo, yeye mwenyewe ni maendeleo (*kicheko*). Yeye mwenyewe ndio maendeleo, yeye ndiyo kila kitu sasa tena atatafuta nini (*kicheko*). Lakini siyo sisi, yeye katika shughuli zake anapotaka, umungu wake unapotaka viumbe kama hawa waonekane, tunavyoambiwa, anasema,"Na awe mtu", mtu huwa. "Na awe mtu", yeye akishatamka, mtu

huwa (*kicheko*). Kutamka kwake yeye, wala si kutamka, kutaka kwake na kutimiza ni kitu kile kile. Lakini japo hivi ndivyo tunavyoamini, lakini Misahafu wala haisemi hivyo. Kwa binadamu ni vigumu kusema hivyo; Misahafu inasema alichukua udongo akaufinyanga finyanga sijui baada ya kufinyanga finyanga akaupumulia, akautia pumzi yake ukawa. Sasa sijui kama ndivyo ilivyokuwa,lakini ma-scientist wanasema sivyo ilivyokuwa (*kicheko*). Ma-scientist wanaokubali Mungu na wasiokubali Mungu wengi sasa nadhani wanakubaliana kwamba hivyo sivyo ulimwengu ulivyotokea wala sivyo binadamu alivyotokea haraka haraka namna hiyo (*kicheko*), ila kwamba uwezo wa kukua ulitumbukizwa katika ulimwengu, na basi, ulikuwa lazima utokee. Ila kinachoacha kushughulika kinafutika, kinaondoka.

Darwin, wale mnaomfahamu, ndio akaanza kuitengeneza tengeneza ile, kutengeneza theory yake na kusema survival of the fittest. Fittest ni katika kazi (*kicheko).* Sasa ikaanza shughuli ya maendeleo. Huwezi kutenga vitu viwili hivi, kuendelea na kazi, kwani kazi ndiyo shughuli ya kuondoa vitu matatizo, kuondoa matatizo yanayomzuia binadamu hali yake kukamilika, na vile vile kuyatumia hayo hayo matatizo, hayo hayo kama ni majiwe. Jiwe wakati mwingine humzuia binadamu kupita, sasa unabomoa, lazima ubomoe, hakuna kusema, "Jiwe toka ahh." Jiwe kutoka kwetu sisi ni kutafuta njia ya kuliondoa, hakuna njia nyingine lazima kufanya kazi. Pili, sio kuliondoa, wakati mwingine unaliondoa halafu, unajua wakati mwingine vitu vingine hufanya kazi, sio kwamba jiwe humzuia binadamu kupita mahala kama lipo lakini huzuia liupepo kuvuma, kuingia huku kama halitakiwi au kuzuia na minyama vile vile, na mijoka na midudu. Kwa hiyo, unaweza ukalitumia lile jiwe, ukajengea nyumba, ukaingia ndani, ukakaa. Moja, ni kuyazuia haya mawe, miti, maji yasituvurugievurugie mambo yetu binadamu. Pili, ni kuyatumia hayo hayo mawe, upepo, maji badala ya kuwa ni mafuriko tu yanavurugavuruga chakula chetu, tuyatumie, yaingie katika mashamba yetu kwa utashi wetu. Tuyaelekeze kiasi gani yaingie katika heka moja hapa, kama ni kwa ngano maji kiasi fulani, kama ni kwa mpunga maji kiasi fulani, na halikadhalika kwa mahindi.

Kwa hiyo, tunashindana na maji, tunashindana na maji haya, kama

yanatuvurugia mambo yetu tunayazuia kutuvurugiavurugia mambo yetu, tunayatumia yatutengenezee mambo yetu. Tunatafuta njia ya kutengeneza nguvu ya umeme badala ya kuweka punda au sisi wenyewe ndio tunazungusha lidynamo. Kwa nini sisi tuzungushe lidynamo? Tunaanza kutumia akili. Kazi tunajuani lazima, kazi kama lazima dynamo lizunguke kwa sababu hakuna namna nyingine ya kuweza kupata electricity. Kwa hiyo nasema, kwa nini sisi tukae hii mimaji ina nini, hii mimaji ina nini, tukae tunaitumia kutengeneza namna jinsi mimaji inavyokuja tunapata electricity. Na kila mnavyozidi kufanya kazi kwa akili zaidi ndivyo mnavyozidi kwenda, ndivyo mnavyozidi kuendelea. Maendeleo na kazi – kazi ni physical na kwa akili zaidi, na kwa vyombo tunavitumia, tunatafuta vyombo vya kutusaidia kufanya kazi vizuri zaidi. Ndio ubinadamu wenyewe, ndio maisha yenyewe, ndio uhai, ndio maendeleo, ndio civilization, ndio utu, hakuna namna nyingine. Hakuna utu, hakuna heshima zaidi. Sasa tutakuheshimu vipi hufanyi kazi? Hii ni kitu cha maumbile ya mtu na namna yake ya maendeleo, sisi binadamu, hiyo ndio namna yake ya kuendelea.

Sasa hii inakwendakwendaje basi! Maana yake kama kazi ndio utu, kama kazi ndio maendeleo, kama kazi ndio maisha, ni uhai, kazi ndio civilization, ndio uungwana, ndio kula vizuri, ndio kuvaa vizuri, ndio kuishi katika nyumba nzuri, ndio kutembea kwa ndege, ndio kushinda matatizo yote tuliyo nayo duniani - namna ya kuyashinda ni kazi; kama hivi ndivyo, kazi imekwendakwendaje tena hata ikawa ni kitu cha dharau dharau? Ukiitwa mfanyakazi lo! Inakuwa kama kwamba hukuitwa binadamu. Ukiitwa mfanyakazi kama ni aibu na kumbe kuitwa mfanyakazi ndio kuitwa binadamu. Sasa imekwendakwendaje, hapa katikati imekwendakwendaje? Vimetokea vijambo hapa katikati vikavuruga heshima ya kazi.

Moja utumwa, moja utumwa, binadamu kummiliki binadamu mwenzie, kitu binadamu anammiliki binadamu mwenzie. Kazi sasa, huyu binadamu anafanya kazi, kazi inaacha kuwa sasa ni kitu cha maendeleo ya binadamu. Ninapokuwa mimi mfanyakazi inajulikana kwamba nafanya kazi kwa maendeleo yangu na wenzangu. Inakuwa sasa kazi ni kitu namfanyia fulani. Ninyi mmekwisha kuwa mali ya mtu, mnamfanyia kazi; ananituma na

nisipofanya kazi ananitandika au ananiuwa. Mimi nimekuwa kama ng'ombe wake. Binadamu anafanya kazi kama ng'ombe, kama punda, mimi nakuwa chombo cha mtu, naacha kuwa binadamu. Sasa na kazi yangu hii naifanya, nafanya kama chombo kama linavyozunguka lile panka. Kazi ile tena na ubinadamu wangu vinatengwa, kazi na ubinadamu wangu vinatengwa kwa sababu nimekwishafanywa chombo cha mtu, huyu anayeniambia fanya kazi. Sio ubinadamu wangu ni fedheha ya kutawaliwa ndio inanifanya nifanye kazi, siyo ubinadamu wangu, vimetengwa vile, ubinadamu wangu, utu wangu na kazi yangu kwa sababu ya utumwa. Kitu kimoja kilichoanza kuvunja heshima ya kazi: Utumwa na heshima ya binadamu havipatani. Na kazi ya kitumwa si kazi ya maendeleo ya binadamu, ni kazi ya kumfaidisha mtu. Inaweza ikaleta maendeleo vile vile, si kama haileti maendeleo, inaleta maendeleo. Warumi wametumia watumwa sana, wameweza kuleta maendeleo ya aina fulani makubwa lakini maendeleo hayo ni maendeleo katika aibu. Kazi nia yake siyo kuleta maendeleo katika aibu, siyo. Ni kuleta maendeleo kwa heshima. Utumwa ni kitu cha kwanza kilichovunja heshima ya kazi.

Kitu cha pili kilichovunja heshima ya kazi ni ubepari- capitalism. Utumwa - mtu anammiliki mtu. Capitalism, ingawa inadhaniwa nzuri zaidi, wakati mwingine inadhaniwa labda si utumwa sana, lakini hata ni ngumu zaidi kueleza. Katika kazi ya heshima, katika kazi tunayofanya tunatumia vyombo - tunatumia jembe, tunatumia shoka, tunatumia panga. Baadaye mambo yanaendelea tena unaweza ukatumia mashini mambo yanazidi kuendelea, vyombo tunavyovitumia binadamu.

Binadamu anatumia chombo - anatumia shoka, anatumia panga, anatumia mundu. Binadamu anavifanya hivi vyombo, baada ya kuvifanya, anavitumia vimsaidie katika shughuli zake. Hiyo ndiyo kazi ya kawaida, ndiyo kazi inayojulikana.Mnaoamini Mungu aliyoitaka Mungu, au mnaoamini maumbile tu hivi hivi tu basi yanayotaka maumbile. Binadamu anatumia vyombo. Kama hana cha kwake anaazima kwa mwenziwe. Kama wewe una mashoka mawili niazime maanamimi sina shoka leo. Ananiazima shoka nikafanyie kazi. Inajulikana shoka ni kitu anachotumia binadamu kwa kufanyia kazi.

Mwenzangu kama wewe una shoka mimi sina, unaniazima tu. Ma-capitalist wamegeuza hii. Ma-capitalist wanageuza hii. Mashoka yanaazima watu (*kicheko*). Badala ya watu kuazima mashoka, mashoka yanaazima watu. Mashoka yamekaa palepale sasa yanasema "Wewe una watu yahe?" "Eeh niazime watu."

Kuna watu hivi sasa mashoka yanawatafuta. Yapo, kuna kitu kinaitwa capital kinatafuta labour (*kicheko*). Ikawa sasa badala ya watu hawa kusema "Bwana niazime shoka; bwana una shoka niazime likafanye kazi, mimi binadamu, binadamu hufanya kazi, hufanya kazi kwa mkono, lakini kufanya kazi kwa tu hivi hivi aah, niazime shoka lako." Unaweza ukaniambia "Tayari ukishalima kule shoka langu bwana eeh, unaweza kunipatia mtama kidogo." "Nitakupatia bwana. Nitakupatia, hiyari kabisa nitakupatia mtama." Lakini hapana. Ananiambia, "Tazama, nina shoka, sasa njoo kwangu, ndiyo. Madhali mimi nina shoka wewe huna, wewe njoo kwangu." Kisa? "Mimi nina shoka." Sasa mimi nakwenda kwa huyu, utumwa wa namna nyingine. Mimi nakwenda kwa huyu nakaa naye, ana vyombo mimi sina, nafanya kazi kwake. Ananimegea chakula, nashiba kiasi, lakini akipenda nishibe. Mara nyingine atanipa kiasi cha kushiba kidogo, basi, hapana zaidi. Maana zaidi nitafanya jeuri. Ananipa kiasi cha kushiba kidogo, basi. Inayobaki, kutokana mimi ndiye mshika shoka, nalima ananigawia kidogo nile; inayobaki, kama nitaongeza shoka, yake. Akiongeza matatu, yake. Akiongeza manne, yake. Kutokana na nguvu yangu ile, si nguvu yangu naiona mimi nataka shoka moja tu, sasa tangu nianze kulima huyu keshapata matatu, siwezi kudai shoka moja katika hayo kama langu aah. Kila mashoka yatakavyopatikana huyu mheshimiwa anachukua tu *(kicheko)*. Mashoka yote yanakwenda kwake. Na kazi mimi ndiye ninayefanya. Mimi nafanya kazi, nazaa mashoka na brain anachukua. Pengine hana chochote huyu ana vishoka tu. Ndiyo. Anachukua designer safi, anachukua engineer safi, anamchukua scientist safi kabisa, anatulipa huyu mwenye mashoka huyu. Sisi wenye nguvu, wenye brains anatulipa huyu. Pengine hajui chochote, analo shoka tu basi (*kicheko*). Na kila tunavyopata yeye ndiye mgawaji (*kicheko*). Je, mliona wapi? Hakuna mfanyakazi akawa millionaire bwana. Millionaire anakuwa ni mwenye

mashoka tu. Kila tukizidi kinachoongezeka anachukua, anachukua.

Kazi ikawa ni kitu kinamfanya mfanyakazi ananung'unika. Kitu ambacho kilitakiwa, mfanyakazi unung'unikeje na kazi ndio uhai, kazi ndio maendeleo, kazi ndio utu, kazi ndio heshima? Ilikuwa kila unapozidi kufanya kazi, kila ukipata pesa yako unafurahi. Ukitengeneza meza unafurahi kwa kawaida ya kazi. Unaitoa hiyo aah. Tena unaona kama utu wako, kama vile Mungu anavyoumba, kila yanavyopatikana mabinadamu mengi haya unaona labda Mungu nadhani anafurahi. Sijui hufurahi Mungu, lakini nadhani Mungu hufurahi *(kicheko)*. Na wewe binadamu kila unapofanya kazi, na kazi ile ikatoa meza kama hizi, ikatoa saa, ikatoa nguo yule tailor anavyokatakata akaishona akakuwekea ikapendeza, anafurahi, lazima. Matokeo ya kazi ni furaha, matokeo ya kazi hayawi manung'uniko. Mtu mfanyakazi tena ananung'unika kutokana na kazi yake, vipi nitanung'unika? Huyu ndiye anayefanya sana kazi, inakuwaje kitu manung'uniko? Sasa unategea. Lazima utegee bwana, ala! Kwa nini hili linanipa shida? Mimi mfanyakazi nalipwa mshahara kidogo tu. Sasa unaanza kutegea. Hufanyi tena kazi kwa sababu unaona kazi ndiyo utu, ndiyo maisha, ndiyo civilization eh, hata kidogo. Capitalism, Ubepari. Kitu kimoja kilichovunja heshima ya kazi.

Kwanza nasema utumwa, mtu kummiliki mtu. Halafu ubepari, mali kuajiri mtu, kuazima mtu. Siyo kusema eti kuazima basi, kutawala hasa. Kutawala hasa. Mali inatawala mtu badala ya mtu kutawala mali. Mashoka yanakuwa, katika viwili hivi, huyu anatumia shoka, kikubwa eti kinakuwa ni shoka. Ubishi unapotokea mali hii achukue nani, tunaamua lichukue shoka. Siyo achukue mtu. Hilo la pili kilichofanya kazi iwe haina maana.

Ya tatu ndiyo ya mwisho, sijui kama kuna kingine. Ya tatu, ya mwisho ni Ukoloni. Nchi kumiliki nchi ni namna ile ile. Ndiyo hali ya mwisho ya utumwa ule au na ubepari, nchi kumiliki nchi. Nchi inamiliki nchi nyingine. Nchi moja inamiliki nchi nyingine, inaitumia nchi ile kama vile Waingereza walivyotumiliki vile, hawa hapa mtulimie basi. Kuna watu kazi yao ni mitemba tu, hawafanyi kazi, inakuwa kuna heshima, eti kuna heshima kuvuta mitemba (*kicheko*). Kuna heshima kuvuta mitemba, heshima? Heshima ni

kazi, heshima ni kazi. Leo kuna heshima ya mitemba tu? Basi ukoloni taifa moja linavamia taifa lingine linawatawala au kitumwa au kibepari. Sisi hawa walitutawala kibepari, tunawafanyia kazi. Kwa hiyo lazima tunung'unike na kazi ile. Si kazi kama kazi ilivyokusudiwa iwe, mnh mnh, ni kazi ya kuwafaidia hawa jamaa. Si kazi kama nia ya kazi ilivyo; kama kusudi la kazi lilivyo, linamfaa yule mfanyakazi mwenyewe au inafaa umma mzima, kwa sababu ni faida ya mtu au umma kwa jumla. Kazi, namna yake inavyotakiwa, hapana, inakuwa kwa huyu, kwa mfanya kazi mwenyewe ina faida yake minimum,kwa umma haina. Haina. Ina faida kwa kikundi tu kinachotawala kinawakorofisha. Kazi ikawa haina heshima. Ikavurugika kazi.

Sasa, baada ya kupiga soga hilo mheshimiwa, tunarudi kwenye *Azimio la Arusha* na *Education for Self-reliance. Education for Self-reliance* lazima ifanye kazi mbili, ina shabaha mbili. Moja, nikufuta mawazo yale ya kitumwa, ya kibepari na ya kikoloni juu ya kitu kazi. Kazi yake moja ni kuyafutafuta moja kwa moja mpaka tusiwe na mwalimu na mwanafunzi na kiongozi wa TANU au na Mtanzania yeyote ambaye ana mawazo ya kitumwa, ya kibepari au ya kikoloni juu ya kazi (*makofi*). Ndiyo kazi yetu ya kwanza ya kufuta yale mawazo yetu tuliyokuwa nayo ya hovyo, kwamba, kupewa elimu, kwamba ni kuepushwa kazi. Jambo la kijinga sana! Anaweza mtu anayesoma katika namna ya kikoloni au ya kitumwa au ya kibepari, unaweza kumuuliza, "Nia ya kwako unasoma kwa nini?" "Niepuke kazi bwana." Aepuke kazi ngumu, aweze kuvuta mtemba, akala kwa kuvuta mtemba tu na kuona watu wengine wanafanya kazi. Ni kufuta kwanza mawazo yale. Lazima kuyafuta yale mawazo ya kijingajinga yale. Ni mawazo dhahiri ni mawazo ya kijinga.

Pili, hiyo moja ni negative tu kufuta machafu. Kufuta machafu positively kuweka mahala pake, kuirudisha kazi mahala pake, heshima yake. Heshima yake ndiyo utu, kwamba mtu nafsi yake hawezi akakua, atabaki hivi hivi hakui, atavia, hakui ikiwa hafanyi kazi. Hawezi akakua. Kiungo chako kimoja au kama ni akili au ni kiwiliwili hakitakuwa, hakitakomaa ikiwa hutafanya kazi. Dhahiri kabisa, vipi akili yako ikue bila kufanya kazi? Haiwezekani. Na vipi mwili wako ukue bila kazi? Hakuna, lazima ufanye

kazi. Yale madudu yanayotupiga ngumi yale kama kina Cassius yale, ala, yule anaufanyisha kazi sana mwili ule. Wewe unafikiri ni tani tu basi ukilichukua jitu jingine nalo ulipime uzito ukiliona uzito ni sawasawa kama Sheikh Walwa hivi (*kicheko*). Halafu umwambie Sheikh Walwa "Basi wewe na Cassius uzito wenu ni sawasawa, haya" (*kicheko*). Hakuna! Hakuna hata kidogo, ni mbalimbali itakuwa kama mtoto mdogo eeh. Kwa sababu hili ni limwili la kazi, kazi kweli kweli hili. Ngumi moja tu inaweza kuleta balaa. Mwili lazima ufanye kazi. Mwili gani utalala tu na kuvuta sigara tu basi? Na nani, na nani, mpumbavu gani anataka mwili wake unavuta sigara tu. Mwili lazima ufanye kazi, lazima,lazima kabisa. Huu ni ujinga, ni jambo la ajabu, ni jambo la kipumbavu sana kudhani mtu anakuwa mtu kwa kulala tu kutwa kucha kitandani. Laleni tuone. Eh, muachwe mulale tu tuone kama mtakuwa watu. Kwanza hamtapendeza, nasema hamtapendeza. Ndiyo, mtakuwa matufetufe tu hivi hivi (*kicheko*). Mwili gani? Mwili wa binadamu ule uwe unakula tu, unakula tu haufanyi kazi, utakuwa tufe tu. Hauwezi kupendeza, kwa namna yeyote hauwezi kupendeza. Mwili wa binadamu lazima ufanye kazi, ndiyo namna yake.

Kadhalika, akili ya binadamu lazima inolewe kama upanga unavyonolewa. Na namna ya kuinoa ni kuifanya ifikiri, na hakuna namna ya kufikiri bila kazi. Eh wanavyoniambia rafikiri zangu Wahindi eh, wanayo dini yao wanasema una life of contemplation (*kicheko*). Sasa eti una-contemplate. Una-contemplate eh, you can't, uta-wither, you will wither away, utakwisha, una-contemplate. Eti unamsogelea Mungu kwa contemplation, no, no, no (*kicheko*). Mtu amsogelee Mungu, hata tunaoamini kwamba kuna Mungu hatumsogelei Mungu kwa contemplation, kitu kinaitwa pure contemplation, hata kidogo. Unamsogelea Mungu katika activity. Hakuna namna nyingine ya kumsogelea Mungu. Mungu tunavyomjua sisi, tunavyomjua acha namna nyingine, kama Mungu yupo namna ya kumjua ni creator. Ni creator. Ni creator, aliyekuumba wewe, aliyeumba nyota, aliyeumba ulimwengu, ndivyo tunavyomjua. Mengine yale tunayoambiwa tuna-conclude tu kwamba vile vile ni mpenzi *(kicheko).*

Hayo tunayoambiwa, na tunaona labda reasonable, kwa nini atuumbe kama

alikuwa hatupendi? Kwa hiyo lazima anatupendapenda na tunaona kama reasonable enh. Lakini kitu kimoja ambacho ni dhahiri kabisa ni creator, ni worker. Ndiyo. Sasa namna yake ya kufanya kazi labda tofauti na yetu, lakini utamsogelea Mungu eti by contemplation (*kicheko*). Aah! Hii brain ya mtu sijui uiweke wapi ya contemplation tena uifungie mahala. Uifunge mahala itokane na ulimwengu mwingine wote, ifike mahala ina-contemplate tu. Mnh! This is rubbish. Binadamu namna yake ya kumsogelea Muumba wake ni kwa kazi, basi; hakuna namna nyingine (*makofi)*. Ni kwa kazi ndivyo tunavyoweza kushindana na ma-obstacles haya. Haya yaliyomo duniani; haya yanayotusumbuasumbua, yanazuiazuia maendeleo yote. Ndiyo maana akina Marekani hawa wanakwenda kwenye mwezi.

Nilipata kusema juzi hapa sasa kama kule kwenye mwezi kweli kungekuwa na Wazaramo kule wanaliona hili dudu la Marekani linafika pale vupp, linaanza kuchimba, mara linaanza kuchimba, si wangesema limetumwa na Mungu hili! (*kicheko*). Halafu wangesemaje? Wazaramo hawa kwenye mwezi, hili dudu linakuja linaanguka vupp, eeh eeh, halafu wanaona lenyewe tu linachimba, linachimba; la nini? Limetokea wapi? Limetokea huko, na ndivyo kweli. Wanasema huko kuna brains. Kuna brains ndiyo imeleta hii hapa, ndiyo ikaanguka hapa. Halafu baada ya hapo ni brain ile ile inayoiambia chimba sasa. Sasa Mzaramo asiseme limeletwa na Mungu bwana enh? Na hivyo ndivyo jinsi ya binadamu, kama kuna Mungu wao namna ya kumkaribia ni kufanya vitu vya namna hiyo, ni kufanyakazi siyo contemplation. Contemplations zitakugundulisha siri za Mungu, siri za Mungu lazima uchimbe chini pale. Hakuna namna nyingine ya kujua. Unachimba kama unatafuta mafuta chini pale, unachimba. Hakuna ku-contemplate to find kama kuna mafuta pale chini (*kicheko*).

Maana ingekuwa hivyo ndivyo, well, kama kuna new contemplator anatuambia kuwa kuna mafuta pale chini a-contemplate tuweze kulitengeneza limto letu hili tufanyie electricity; a-contemplate twende kwenye mwezi, wee! (*kicheko)*. Maneno ya kijinga sana haya! Namna peke yake ya binadamu anavyoweza eh, ambavyo kweli uwezo wa binadamu hauna kikomo. Uwezo wa binadamu kwa upande mmoja hauna kikomo. Uwezo wa binadamu kwa

pamoja, siyo binadamu mmoja mmoja. Binadamu mmoja mmoja hawana uwezo mkubwa sana. Uwezo wa binadamu kwa umoja wao, katika historia yao, hauna kikomo. Hauna kikomo.Siyo kwamba wanakwenda kwenye mwezi tu, wanakwenda kwenye kila nyota iliyomo duniani, inayoweza kufikiwa, iliyopo katika ulimwengu wataifikia. Na kama hazina kikomo, basi watakuwa wanatoka nyota hii wanakwenda hii, nyota hii wanakwenda hii, bila kikomo, watakwenda tu. Hakuna namna ya kumzuia binadamu, ni kwa kazi na akili. Brain ile inachanganywa na physical work na hakuna namna nyingine ya kukwepa. Nasema hiyo ndiyo KAZI. Hivyo ndivyo heshima ya kazi.

Sasa lazima kusema kweli ivurugike vurugike sana. Na maana yake nini? Kwa jumla nini? Maana yake kwa kifupi ni nini? Kwamba kitu utumwa hakina heshima kwa binadamu, lazima kifutwe kama binadamu anataka kuendelea. Lazima kifutwe. Kwa sababu kina-interfere na method yenyewe ya mtu kukua. Kitu kama utumwa lazima kifutwe kama unataka binadamu waweze kwenda. Kitu ubepari lazima kifutwe. Lazima kitafutwa kwa sababu kinavurugavuruga method yetu ya kuwa Vimungu vidogo. Vinatuvurugia hapa. Ubepari, kitu kama ubepari kinatuvurugiavurugia hapa, kinataka kitufanye tuanze kunung'unika nung'unika; na kitu kama ukoloni koloni huu lazima ufutwe. Sasa elimu yetu wananchi mimi nasema, kama tunataka elimu yetu iwe ni elimu barabara, isiwe elimu ambayo matokeo yake ni kwamba ukimwambia mtu "Fanya kazi" anasema "Unanitukana." Aah! Kinyume kabisa cha hali hiyo. Binadamu we vipi wewe, fanya kazi, tena iwe kuna kazi eti ya waungwana na kazi nyingine si ya waungwana. Kazi ni ya watu. Kazi ni ya binadamu tu. Na anafanya iliyopo. Kama kazi yenyewe ni ya kutengeneza meza unatengeneza. Tena bahati mbaya sana, watu wengine hatukufundishwa; unajuta mtu sikufundishwa kutengeneza meza. Mimi sijui kushika nyundo. Emmanuel* vile vitu tukitengeneza we bado unakumbuka? (Ndiyo) Wewe bado unakumbuka mwenzangu? (Bado nakumbuka). Enh, tulikuwa tunatengeneza stools, stools hizi sasa bwana uje unionyeshe mwenzangu (*kicheko*). Mimi leo nikishika nyundo,

* Yumkin huyu alikuwa Emmanuel Ndonde, mmoja wa wanastudy-group.

nitajivunja kidole. Lakini, sasa niambiwe “Julius, njoo tukufundishe jinsi ya kutengeneza meza,” niseme mnanitukana? Mimi President wa Tanzania mnanitukana? Mnaniambia nijifunze kutengeneza meza mimi? Eh wewe! Mimi President mzima unaniambia unifunze kutengeneza meza mimi! *(kicheko).* Dharau. Unaniambia nitengeneze meza mimi? Au nikionekana mimi natengeneza meza, niko mahala nina randa yangu na najitengenezea meza, si watasema huyu President gani huyu?”Anatengeneza meza?” Nyumbani mwangu ningekuwa nimefundishwa, sikufundishwa. Lakini ningekuwa nimefundishwa mimi, ingekuwa elimu niliyofundishwa si ya kijingajinga hii, ingekuwa nimefundishwa naweza kutengeneza electricity nikivurugiwa vurugiwa, naweza kuitengeneza. Niambiwe huyu President gani huyu anafanya kazi! Electricity nyumbani kwake ikiharibika, eti anatengeneza mwenyewe. Na majitu chungu nzima yanaweza kumtengenezea, eti anatengeneza mwenyewe. Hiyo iwe navunja heshima? Kuna kazi isiyo na heshima? Ni kazi gani, ukiondoa mawazo ya kijingajinga haya, ya kitumwa haya, ya kibepari, ya kikoloni, kazi isiyo na heshima ni kazi gani?

Nikikoga mimi katika bafu langu mwenyewe, nikilisafisha najivunjia heshima? Heshima yangu ni kupata mtu wa kuja kunisafishia bafu! (*kicheko*). Ashakum, kuna mambo mengine nikifanya nikivuta hivi, navunja heshima hivyo? *(kicheko).* Eee! Kuna kazi gani isiyokuwa ya heshima ukiondoa, ukishafuta mawazo ya kitumwatumwa haya, na mawazo ya kibepari na mawazo ya kikoloni, kazi isiyokuwa ya heshima ni ipi? Nikilima, nikiwa shambani nalima mpunga navunja heshima, Mheshimiwa eeh? Sasa, heshima inavurugika maana nalima! Eee!

Nasema, haya ni mawazo ya kijinga - ya watumwa na wafugaji wa watumwa; ya mibepari na ya wakoloni; lakini si mawazo ya kibinadamu sawasawa.

Waheshimiwa nimekwisha piga soga, inatosha, nawatakieni heri katika mazungumzo yenu (*makofi*).

# 3

## Kuishi Pamoja

Kuishi kijamaa ni kuishi pamoja na kufanya kazi pamoja kwa faida yetu wenyewe. Kijiji cha ujamaa ni kikundi cha watu wanaoishi pamoja na kufanya kazi pamoja kwa faida yao wenyewe.

Kuishi pamoja, yaani kuishi katika kundi, ni tabia ya binadamu na wanyama wengine wengi, wa nyumbani na wa porini. Lakini tofauti ya kuishi pamoja kwa binadamu na kuishi pamoja kwa wanyama ni kubwa kiasi kile kile cha tofauti baina ya binadamu na wanyama. Mnyama akiwa katika kundi ni mmoja tu katika kundi. Si "fulani" katika kundi. Japo angapewa jina ni kama la bandia tu. Hana nafsi, hajijui, hajiiti "mimi''. Hana uhusiano kati yake na wenzake ambao ni uhusiano wa nafsi; yaani uhusiano wa kiumbe anayejijua na kujiita "mimi", na kiumbe mwenziye ambaye pia anajijua na kujiita "mimi".

Vile vile uhusiano wao na ulimwengu na mazingira yake ni uhusiano wa kimaamuma tu. Kwa kuwa hawajijui basi hawaujui ulimwengu. Uwezo walionao wa kubadili mazingira ya ulimwengu ili yawasaidie katika maisha yao ni uwezo mdogo sana; tena hauongezeki wala haupungui. Simba anavyowinda leo ndivyo alivyowinda jana na ndivyo atakavyoendelea kuwinda hadi mwisho wa dunia. Na tembo, na nyati, na nguchiro, na mamba na mkizi, na nyuki, na mchwa, mwewe na kanga; wasipobughudhiwa na binadamu au kufutwa duniani, vile walivyoishi jana ndivyo wanavyoishi leo na ndivyo watakavyoendelea kuishi mpaka mwisho wa dunia.

Lakini binadamu ni tofauti. Binadamu ana nafsi. Anapokuwa katika kundi si mmoja tu katika kundi: ni Fulani bin Fulani, au Fulani binti Fulani, katika kundi. Anajijua, na jina lake la kwanza kabisa ni "mimi", na hili si jina

la bandia, maana ndilo linalomfanya tofauti na wanyama. Kwa ajli hiyo, anapokuwa katika kundi pamoja na wenzake, si mmoja tu katika kundi; bali ni "mimi" pamoja na kina "mimi" wenzangu. Binadamu anatambua, au angalau anapaswa kutambua, ubora wa nafsi yake; na kwa ajili hiyo anatambua, au angalau anapaswa kutambua, ubora wa kina mimi wenzake, kwani wao ni mfano wake na yeye ni mfano wao. Kwa hiyo kuishi pamoja kwa binadamu ni tofauti sana na kuwa pamoja kwa kundi la wadudu "walioendelea" kama mchwa au nyuki. Kuishi pamoja kwa binadamu ni kuishi kwa pamoja kwa viumbe wanaojijua na kujuana; na ukubwa wa kujuana kwao unatokana na ukubwa wa kujijua kwao.

Aidha, kwa sababu binadamu anajijua, anaujua ulimwengu na mazingira yake. Na kila anavyozidi kujijua ndivyo atakavyozidi kuujua ulimwengu na mazingira yake. Na uwezo wa binadamu wa kuujua ulimwengu na kutumia ujuzi huo kwa maendeleo ya binadamu hauna kikomo. Lakini uwezo huo usiokuwa na kikomo ni wa binadamu katika kushirikiana, binadamu mmoja mmoja hana uwezo mkubwa sana. Binadamu bila wenzake ni kweli anayo tofauti kubwa ajabu na wanyama, yeye ni "mimi" na wanyama si kina "mimi". Hii tofauti ya hulka au maumbile imebaki japo kama binadamu yuko peke yake. Lakini katika kitu kinachoitwa maendeleo, au ustaarabu, au utamaduni, hakuna tofauti kubwa kati ya mnyama na binadamu anayeishi peke yake. Hawezi kuwa na nyumba nzuri, ataishi katika shimo au pango; hawezi kulima, wala kufuga; atakula mizizi, asali au nyama ya wanyama wa porini, hawezi kuvaa kwa sababu hana haya, na akivaa atavaa majani au ngozi. Hawezi kuwa na lugha, kwa sababu lugha ni chombo cha kubadilishana mawazo kati ya "mimi" na 'mimi' mwingine. Binadamu peke yake hata angeishi milele hawezi kufanya maendeleo yoyote - atabaki mshenzi milele. Kuishi pamoja ndiyo hatua ya kwanza ya maendeleo.

**Binadamu na Kazi**

Kabla ya kuendelea kueleza kanuni ya pili ya maisha ya kijamaa, yaani kufanya kazi pamoja, ningependa kwanza kutoa maelezo mafupi juu ya kazi. Nafanya hivi hasa kwa sababu baadhi ya ndugu zetu, na pengine binadamu kwa jumla, hudhani kuwa kazi ni balaa. Kazi si balaa; kazi ni baraka. Kazi ni baraka kwa sababu uhai ni baraka; na uhai ni kazi. Mauti ni mwisho wa kazi. Kutamani kutofanya kazi ni kutamani mauti: yakija utajuta!

Mtoto azaliwapo tukitaka kujua kama kazaliwa hai tutachungua tuone kama viungo vyake vinafanya kazi. Kwa kweli akizaliwa hai hatasubiri mpaka tuchungue, yeye mwenyewe atatuambia kuwa kazaliwa hai; na hutuambia kwa viungo vyake vinavyotoa sauti - ATALIA. Na akilia mama yake atafurahi, maana atajua kuwa mtoto kazaliwa hai. Na kama kazaliwa na afya kamili, basi viungo vyake vyote vitakuwa vinafanya kazi barabara. Ni mama maluuni ambaye atatamani mtoto wake azaliwe na viungo vyake havifanyi kazi barabara; maana mama huyo atakuwa anatamani kuzaa maiti. Basi, kuzaliwa hai ni kuzaliwa unafanya kazi, na unaifanya barabara.

Kadhalika, kuendelea kuwa hai ni kuendelea kufanya kazi na kuifanya barabara. Mtoto lazima aendelee kulia, kunyonya, kwenda haja na kufurukuta. Moyo wake lazima uendelee kupigapiga, damu yake lazima iendelee kutembea mwilini; mishipa yake ya damu lazima iendelee kupitisha damu. Mapafu, mafigo, matumbo na kila kiungo chake cha mwili lazima kiendelee kufanya kazi, kwani hiyo ndiyo maana ya kuwa hai. Hakuna mama mwenye akili ambaye atafurahi sana akiamka siku moja na kugundua kuwa viungo vya mwili wa mwanae vinaanza kuacha kufanya kazi, maana hii ni dalili ya kuanza kufa.

Mtoto humtegemea mama yake. Mama yake hana budi amlishe; asipomlisha, mtoto atakufa.

Lakini hata mama humlisha mwana matunda ya kazi, japo kama ni maziwa ya matiti yake mwenyewe. Bila kazi yake mwenyewe au kazi ya mtu mwingine yule mama asingekua hata aweze kuzaa mtoto, achilia mbali kule kupata afya

na maziwa ya kumnyonyesha mtoto. Lazima ilifanyika kazi, na inaendelea kufanyika, ndiyo maana mama anapata chakula. Hata kama kazi hiyo ni ya kuokota tu matunda au majani ya porini, au ya kuyatia kinywani tu na kuyatafuna, kuyameza na kuyayeyusha mwilini na kuyageuza yawe maziwa; yote hiyo ni kazi. Shughuli hizo zikifika tamati, na uhai umefika tamati; na mtu yeyote asiyekuwa baradhuli, hatamani zimalizike, ila kwa sababu yake mwenyewe, awe anatamani mauti.

Daktari anapotoa hati ya kuthibitisha kwamba mtu fulani kesha kufa, kwa kweli anatoa hati ya kuthibitisha kuwa viungo vyake vyote pamoja na ubongo wake, vimeacha kufanya kazi. Hiyo ndiyo maana ya kufa. Kuogopa kazi ni kuogopa uhai; maana uhai ni kazi. Kutamani kutofanya kazi ni kutamani kufa; maana kufa ni kukoma kabisa kufanya kazi. MAUTI NI MWISHO WA KAZI, au tuseme MWISHO WA KAZI NI MAUTI.

Lakini hata kwa mtoto kuwa hai peke yake hakutoshi. Ikiwa afya ya mtoto ni nzuri kabisa tunatazamia kuwa kila siku atafikia hatua ya juu zaidi katika maisha yake. Hawezi kujiongezea (wala kujipunguzia) ubinadamu wake. Leo hawezi kuwa binadamu zaidi kuliko alivyokuwa jana; na wala kesho hawezi kuwa binadamu zaidi kuliko alivyo leo. Lakini kama afya yake ni safi, basi uwezo na vipawa vyake vya kibinadamu vitazidi kukamilika kila siku. Viungo vyake vitaendelea kukua, akili zake zitaendelea kukua. Na kukua ni kazi, na hufanyika tu katika kazi, na wala hakuna mwisho. Hasa yenyewe; na kazi wanayoiogopa zaidi kupita zote ni kazi ya kufikiri, maana kwao ni ngumu. Wangefikiri kidogo tu wangetambua kwamba wanachotaka ni kufanyiwa kazi, na kwamba ikiwa wao wanaona kuwa kujifanyia kazi ni karaha basi wengine wataona kuwa ni karaha zaidi kuwafanyia kazi makupe. Lakini naona nakimbia mno, sijafika kwenye visa vya makupe bado. Jambo nililojaribu kulieleza ni kwamba kazi ni kitu cha lazima kwa binadamu kwa sababu uhai ni kazi na kazi ndiyo uhai.

**Kufanya Kazi Pamoja**

Tumekwisha kuona kuwa ili binadamu aendelee kuishi hana budi afanye kazi. Kwa kweli tumekubaliana kwamba uhai ni kazi; yaani kuishi na kufanya kazi maana yake ni ile ile. Tumekubaliana pia kwamba, kuwa hai haitoshi. Uhai, hasa uhai wa binadamu, lazima umsaidie kukua. Na kwa binadamu kukua maana yake siyo kuongezeka uwezo wake wa kuujua na kuutawala ulimwengu na mazingira yake kwa faida yake mwenyewe. Uwezo huu binadamu binafsi hanao mkubwa sana; lakini katika ujumla wao, na wanaposhirikiana, uwezo ambao binadamu wanao wa kuujua na kuutawala ulimwengu hauna ukomo.

Kufanya kazi pamoja ni hatua na sharti la maendeleo. Binadamu ana nafsi; wanyama hawana; pia ana ubongo mkubwa zaidi wa kuleta maendeleo zaidi kuliko wanyama wengine. Lakini maendeleo ya binadamu si ya maumbile na hulka tu; maendeleo ya binadamu yanaletwa hasa na tabia na mazoea ya kuishi pamoja na kufanya kazi pamoja. Tuseme kila mwanaume na kila mwanamke anayo maumbile na hulka ya kuzaa binadamu wenzake, wanaume na wanawake. Lakini kwa kweli mtoto si tunda la ile hulka tu na maumbile; mtoto ni matunda ya kushirikiana baina ya mwanaume na mwanamke. Na maendeleo ndivyo. Uwezo wa kuleta maendeleo umo, kama mbegu, katika hukla na maumbile ya binadamu; lakini hayaji mpaka binadamu waanze kufanya kazi pamoja.

Hata maendeleo ya wadudu kama vile mchwa na nyuki ni matokeo ya kuishi pamoja na kufanya kazi pamoja.

Ni kweli, kama vile kuishi pamoja kwa nyuki ni tofauti sana na kuishi pamoja kwa binadamu; kadhalika kufanya kazi pamoja kwa nyuki ni tofauti na kufanya kazi pamoja kwa binadamu. Lakini ni kweli pia kwamba hata hayo maendeleo madogo ya ki-mdudu ni matokeo ya wadudu hao kufikia hatua ya kufanya kazi pamoja. Mchwa na nyuki wasingejifunza kufanya kazi pamoja, wasingeweza kujenga hayo maghorofa na miji yao tunayoiita visuguu; wala nyuki kutengeneza asali tunayowanyang'anya. Na binadamu nao wakitaka maendeleo ya kibinadamu hawana budi wajifunze kufanya

kazi kwa pamoja. Kwa wadudu na kwa binadamu sheria ni ile ile. Lazima wafanye kazi pamoja ili walete maendeleo makubwa ya kadri ya hulka yao na uwezo wao. Japo kweli binadamu wao wana nafasi na ubongo mkubwa zaidi kuliko wadudu na wanyama wengine, lakini wasipojifunza kufanya kazi pamoja, maendeleo yao hususan hali ya maisha yao, haitakuwa tofauti sana na hali ya wadudu na wanyama wengine walioendelea.

**Faida yake**

Kufanya kazi pamoja ni jambo la lazima kwa maendeleo kwa sababu mbili kubwa. Sababu ya kwanza, ambayo ni dhahiri zaidi, ni kwamba kufanya kazi pamoja kunaongeza nguvu. Jiwe ambalo lingemshinda mtu mmoja kung'oa au kusukuma, watu wengi kwa pamoja wataliweza. Nyumba ambayo mtu mmoja angechukua mwaka kuijenga, watu wengi kwa pamoja wanaweza wakachukua siku mbili tu; na kadhalika.

Sababu ya pili, ambayo si dhahiri zaidi lakini ni kubwa zaidi, ni kwamba watu wakifanya kazi kwa pamoja wataweza kugawana kazi. Haiwezekani mtu mmoja huyo huyo awe mkulima bora, na pia mhunzi wa majembe, fundi wa kufuma na kushona nguo; kujenga nyumba; kutibu wagonjwa; kusomesha; kutengeneza madawa; kutunga na kuchapisha vitabu; na kadhalika. Mtu mmoja akijaribu kufanya kazi zote hizi hataweza kufanya yoyote. Mtaka yote hukosa yote. Ili kazi hizi ziweze kufanywa vizuri lazima zifanywe na watu mbalimbali. Wengine walime, wengine wafue majembe, wengine wafume nguo; wengine watengeneze madawa; wengine watibu wagonjwa; na kadhalika. Kwa kweli maendeleo makubwa hayawezekani kabisa mpaka watu wamejifunza kugawana kazi.

**Utumwa na Ukabaila**

Binadamu wanaweza kufanya kazi pamoja au kufanzwa kazi pamoja. Maendeleo yanayoletwa kwa kufanzwa kazi pamoja ni maendeleo ya aina fulani; lakini, ni maendeleo ya kitumwa. Matokeo yake huweza yakawa ni vitu kama mabarabara, mapiramidi, majumba makubwa makubwa, na kadhalika. Wasimamizi wa "maendeleo" ya aina hii, yaani wenye watumwa,

huweza kujiendeleza katika mambo ya ustaarabu na utamaduni kama vile muziki, sanaa, uandikaji na kadhalika. Haya ni maendeleo ya wachache. Lakini watu kwa ujumla wao huwa hawana maendeleo yoyote. Kwa kweli, kwa kufanywa kama wanyama wamenyimwa uwezo wowote wa kujiendeleza ki-binadamu na yawezekana hata maendeleo waliyokuwa nayo kabla ya kufanywa watumwa yatapotea kabisa. Kanga hatagi ujani, na wala binadamu haendelei ujani (utumwani). Binadamu haendelezwi kwa kufanzwa kazi, bali hujiendeleza kwa kufanya kazi. Maendeleo ya binadamu, ili yawe maendeleo ya kweli, hayana budi yawe ni matokeo ya kufanya kazi katika hali ya uhuru.

Lakini binadamu wanaweza kuishi pamoja na kufanya kazi pamoja katika hali ya uhuru, kwa faida ya mtu mwingine. Kwa mfano, wafanyakazi katika shamba la mkonge si watumwa. Hata wakati wa mkoloni hawakuwa watumwa. Lakini kwa kweli kazi wanayofanya si yao; maana shamba si lao wenyewe. Wanamfanyia kazi kabaila na yule kabaila anawalipa mshahara kwa kazi wanayomfanyia.

Lakini hata kufanya kazi pamoja kwa faida ya kabaila kunaleta maendeleo; na kwa kweli maendeleo makubwa ya kisasa, hasa katika Ulaya Magharibi na Amerika ya Kaskazini ni maendeleo ya namna hii. Maendeleo tunayoyaona humu nchini mwetu; yaliyoanzishwa wakati wa Mkoloni, yalikuwa ni maendeleo ya namna hiyo. Yaliletwa na watu waliokuwa wakifanya kazi pamoja kwa faida ya makabaila na mabepari. Kufanzwa kazi kwa ajili ya mwingine ni utumwa; na kufanya kazi kwa ajili ya mwingine, japo si utumwa ni unyonyaji. Kama wafanyakazi wanao uhuru wa kutosha basi huunda Chama cha wafanyakazi ili kiweze kuwa kikidai haki zao kwa tajiri wanayemfanyia kazi.

Lakini chama huwasaidia tu kuwapatia kiasi cha matunda ya kazi yao kadiri inavyowezekana. Hakiwezi kuwapatia matunda yote ya kazi yao. Kingefaulu kufanya hivyo tajiri asingepata chochote kutokana na jasho la wafanyakazi, na kwa hiyo asingeng'ang'ania waendelee kumfanyia kazi ambayo haina faida kwake. Kwa hiyo katika utaratibu wa kibepari na

kikabaila chama cha wafanyakazi si chombo cha kuondoa unyonyaji, bali ni chombo cha kupunguza makali ya unyonyaji. Si chombo cha kukata mirija ya wanyonyaji; bali ni chombo cha kuwawezesha wafanyakazi kuikabili mirija ya wanyonyaji na kuipunguzia nguvu zake. Ukabaila unaweza kuzaa maendeleo, na kwa kweli umezaa maendeleo, lakini pia unazaa chuki, kwa sababu msingi wake ni dhuluma. Hakuna jambo jema kwa binadamu kama kusaidiana; maana kusaidiana na kushirikiana ndiyo msingi wa maendeleo ya kweli na msingi wa kupendana. Kwa ajili hiyo hakuna jambo baya kwa binadamu kama kudhulumiana. Mtu kumnyonya mtu, au kumdhulumu mtu ni unyama, ni ushenzi. Ushenzi huu ndio asili ya maafa yote, kama vile baina ya raia wa nchi ile ile; au baina ya nchi mbalimbali; na ndiyo sababu hasa ya ukoloni. Kitu peke yake kinachoweza kuondoa balaa ya unyonyaji katika maendeleo ya binadamu ni sharti letu la tatu la maisha ya kijamaa - kufanya kazi pamoja kwa faida ya pamoja. Kutakuwa na maendeleo makubwa ya vitu na watu. Lakini maendeleo haya yatakuwa ni matunda ya unyonyaji. Kwa hiyo yataandamana na chuki baina ya tabaka ya wafanyakazi na ile ya wanyonyaji.

Maendeleo ya kikwelikweli, ambayo hayana unyonyaji na hayana chuki, lazima yatokane na utawala kamili wa mfanyakazi. Lazima mfanyakazi mwenyewe katika ushirika kamili na wafanyakazi wenzake atawale mali yote ya kijiji au nchi yake. Kila tone la jasho lake lazima limsaidie kwa kutimiza mahitaji yake katika umma.

## Ujamaa

Tulisema awali kabisa kwamba kuishi kijamaa ni kuishi pamoja, na kufanya kazi pamoja, kwa faida yetu. Tukasema, kwa hiyo, kwamba kijiji cha ujamaa ni kikundi cha watu wanaoishi pamoja na kufanya kazi kwa faida yao pamoja. Tumeeleza kwamba kuishi pamoja ni jambo la lazima kwa binadamu, lakini kuishi pamoja peke yake hakuleti maendeleo. Tumeeleza pia kwamba kinacholeta maendeleo ni kufanya kazi pamoja. Tumeeleza maana ya kazi na umuhimu wake kwa binadamu. Tumeeleza tofauti ya kufanya kazi na kufanzwa kazi. Tumesema kuwa kufanzwa kazi kunaleta maendeleo

ya kitumwa; ni maendeleo ya vitu na watu wachache; lakini si maendeleo ya umma. Tumesema, mwishoni, kwamba kufanya kazi kikabaila kunaleta maendeleo ya wachache hata na ya wengi pia, lakini kwa ugomvi, migomo na kufunga viwanda. Ni maendeleo yanayoambatana na dhuluma na chuki. Tumesema kwamba ukoloni, utumwa na vita ni watoto wa ukabaila na ubepari.

Azimio la Arusha linasema:

(a) <u>Katika Nchi ya Ujamaa Hakuna Unyonyaji</u>:

Nchi yenye ujamaa kamili ni nchi ya wafanyakazi; haina ubepari wala ukabaila. Haina tabaka mbili za watu; tabaka ya chini ya watu wanaoishi kwa kufanya kazi, na tabaka ya juu ya watu wanaoishi kwa kufanyiwa kazi. Katika nchi ya Ujamaa kamili mtu hamnyonyi mtu, bali kila awezaye kufanya kazi hufanya kazi, na kila mfanyakazi hupata pato la haki kwa kazi aifanyayo na wala mapato ya wafanyakazi mbali mbali hayapitani mno.

Katika nchi ya Ujamaa kamili watu peke yao ambao huishi kwa jasho la wenzao na ni haki yao kuishi kwa jasho la wenzao ni watoto wadogo, wazee wasiojiweza, vilema na wale ambao, kwa muda, jumuia imeshindwa kuwapatia kazi yoyote ya kujipatia riziki kwa nguvu zao wenyewe.

Nchi yetu ni nchi ya wakulima na wafanyakazi, lakini si nchi ya Ujamaa kamili. Ina misingi ya ubepari na ukabaila na vishawishi vyake. Misingi hii ya ubepari na ukabaila yaweza ikapanuka na kuenea.

<u>(b) Njia Kuu za Uchumi ni chini ya Wakulima na Wafanyakazi:</u>

Namna ya pekee ya kujenga na kudumisha ujamaa ni kuthibitisha kuwa njia kuu zote za uchumi wa nchi yetu zinatawaliwa na kumilikiwa na wakulima na wafanyakazi wenyewe kwa kutumia vyombo vya serikali yao na vyama vyao vya ushirika. Pia ni lazima kuthibitisha kuwa chama kinachotawala ni chama cha wakulima na wafanyakazi.

Njia kuu za uchumi ni: kama vile ardhi, misitu, madini, maji, mafuta na nguvu za umeme; njia za habari, njia za usafirishaji; maji, mabenki, na bima; biashara na nchi za kigeni na biashara za jumla; viwanda vya chuma,

mashini, silaha, magari, simenti, mbolea, nguo na kiwanda chochote kikubwa ambacho kinategemewa na sehemu kubwa ya watu katika kupata riziki zao au kinachotegemewa na viwanda vingine; mashamba makubwa na hasa yale yanayotoa mazao ya lazima katika viwanda vikubwa.

Baadhi ya njia hizi na nyingine zisizotajwa hapa hivi hasa zinamilikiwa au kutawaliwa na Serikali ya Wananchi.

(c) Kuna Demokrasi:

Nchi haiwi ni ya ujamaa kwa sababu tu njia zake kuu au zote za uchumi hutawaliwa au humilikiwa na serikali. Sharti serikali iwe inachaguliwa na kuongozwa na Wakulima na Wafanyakazi wenyewe.

Serikali ya makaburu wa Rhodesia au Afrika ya Kusini ikitawala au kumiliki njia zote za uchumi, hiyo itakuwa ni njia ya kukomaza udhalimu siyo njia ya kuleta ujamaa. Hakuna Ujamaa wa kweli pasipo na Demokrasi ya kweli.

(d) Ujamaa ni Imani:

Lakini Ujamaa hauwezi kujijenga wenyewe. Kwani Ujamaa ni imani. Hauna budi kujengwa na watu wanaoamini na kufuata kanuni zake. Mwana-TANU wa kweli ni Mjamaa, na Wajamaa wenzie, yaani waamini wenzie katika imani hii ya kisiasa na uchumi ni wote wale wanaopigania hali za wakulima na wafanyakazi katika Afrika na popote duniani. Wajibu wa kwanza wa mwana-TANU na hasa kiongozi wa TANU, ni kutii kanuni hizi za ujamaa hasa katika maisha yake mwenyewe. Na hasa mwana-TANU kiongozi hataishi kwa jasho la mtu mwingine au kufanya jambo lolote ambalo ni la kibepari au kikabaila.

Utimizaji wa shabaha hizo na nyinginezo zinazofuatana na siasa ya ujamaa unategemea sana viongozi kwa sababu ujamaa ni imani na ni vigumu kwa viongozi kujenga siasa ya ujamaa ikiwa hawaikubali imani hiyo.

**Maelezo Zaidi**

*Unyonyaji*

Mali ni matunda ya juhudi. Nyumba tunamoishi, chakula tunachokula na nguo tunzovaa, ni matunda ya juhudi. Lazima mtu fulani awaze na kufanya kazi ndipo vitu hivyo vitokee. Kadhalika vitu vingine vyote vya maendeleo ya umma kwa jumla ni matokeo ya juhudi. Shule, hospitali, soko, barabara, kisima kilichochimbwa, na kadhalika, vyote ni matunda ya juhudi. Na wala hakuna namna nyingine ya kuvipata vitu hivi isipokuwa kufanya kazi; na wala hakuna mtu anayeweza kuwa hai, achilia mbali kuishi maisha ya ki-binadamu, bila angalau baadhi ya vitu hivi. Kama basi vitu hivi visipotokana na juhudi yake mwenyewe havina budi vitokane na juhudi ya mtu mwingine.

Chama chetu kinasema kwamba wapo watu wenye haki ya kupata mahitaji yao kutokana na juhudi ya wengine. Watu hao ni watoto wadogo, wazee wasiojiweza, vilema na wale ambao, kwa muda, jumuia imeshindwa kuwapatia kazi yoyote ya kujipatia riziki kwa nguvu zao wenyewe. Sina haja ya kueleza kwa nini ni haki ya watoto na wazee na vilema kutumikiwa na ni wajibu wa umma kuwatumikia. Lakini pengine si rahisi kuelewa kwa nini ni wajibu wa umma kusaidia watu ambao hawana kazi, na wala si kwa kosa lao wenyewe, bali ni kwa kosa la umma.

Mathalani kazi yangu mimi ni ualimu. Ndiyo kazi ninayoweza kufanya vizuri kusaidia maendeleo ya umma, na kupata riziki yangu hutokana na kazi hiyo. Bahati mbaya walimu wamepunguzwa na mimi ni mmojawapo; wala haijulikani ni lini naweza kutakiwa kuendelea na kazi yangu ya kufundisha. Lakini niko tayari kufanya kazi nyingine yoyote. Ni kweli sitaifanya vizuri kama kufundisha, na yawezekana nisiipende kama kufundisha, lakini nipo tayari kujaribu kuifanya vizuri kadri ya uwezo wangu na kuipenda kadri niwezavyo. Wenzangu wanashindwa kunipatia kazi yoyote. Napenda sana kulima; kwa kweli kuondoa kufundisha hakuna kazi nyingine niipendayo kama kulima. Kila kijiji ninachokiendea kinaniambia hakina nafasi kwa mtu mwingine. Najaribu mashamba ya makabaila, na wao pia wanasema

hawana nafasi ya kazi. Naomba serikali inipatie kipande cha ardhi nijilimie mwenyewe. Serikali inashindwa kunipatia ardhi; au inanipa ardhi lakini inashindwa kunipatia jembe wala chakula cha kunisaidia mpaka nipate mavuno ya kwanza. Jembe langu mwenyewe sina wala sina uwezo wa kulipata; chakula changu mwenyewe sina wala sina uwezo wa kukipata; na wala hakuna mtu yeyote aliye tayari kunisaidia.

Ni dhahiri kwamba nikiwa katika hali hiyo sina budi nitunzwe na umma. Nisipotunzwa na umma nitaiba, la, nisipoiba nitakufa. Na nchi yoyote inayomwacha mwenzao kufika katika hali ya kuiba au kufa kwa njaa bila kosa lake mwenyewe ni nchi ya kinyama si nchi ya kijamaa. Ndiyo maana chama chetu kinatufundisha kwamba katika nchi ya ujamaa hasa ni haki ya watoto, wazee wasiojiweza, vilema na jamaa ambao hawana kazi, kutunzwa na umma; na ni wajibu kabisa wa umma kutimiza huduma hiyo. Lakini mtu mwingine hana haki hiyo. Haki yake na wajibu wake ni kushirikiana na wenzake kufanya kazi za kuleta manufaa kwake mwenyewe na wenzake na umma kwa ujumla.

Asiyefanya hivyo, bali anaishi tu kwa jasho la watu wengine ni mnyonyaji. Kama ni tajiri, basi ni kabaila na bepari; na kwa kweli hawa ndio wanyonyaji wakubwa wa duniani - wezi wa mchana. Kama ni maskini mwenzetu, yeye si bepari wala kabaila, ni kupe tu. Lakini kwa kweli naye huwa angepata bahati ya kunyonya wenzake kikabaila angefurahi sana kuitumia. Chama chetu kinataka tukomeshe unyonyaji katika nchi yetu; unyonyaji wa kikabaila na pia unyonyaji wa kikupe.

### *Njia za Uchumi*

Tumesema kwamba mali yote, ya umma kwa jumla, na ya mtu binafsi, ni matunda ya juhudi. Mali yote ni matunda ya mfanyakazi. Makabaila na makupe wanaweza kutumia na kupunguza mali; lakini madhali hawafanyi kazi hawaiongezi hata chembe.

Lakini mtu haumbi kama Mungu. Mtu hawezi kusema "Mali kuwa", ikawa. Juhudi yake haina budi ifanywe kwa vitu vilivyopo na vingine alivyokwisha

kujitengenezea mwenyewe. Vitu hivyo vinatajwa katika Azimio. Vile vilivyopo tu ambavyo havitokani na juhudi ya binadamu ni vitu kama ardhi, misitu ambayo haikupandwa na watu; madini au mafuta yaliyo chini ya ardhi, n.k. Vitu hivi ni mirathi ya wananchi wote, si mali ya mtu au kikundi cha watu. Vitu vya pili ni vyombo vya kufanyia kazi. Kiwanda, kwa mfano, ni jumba lenye mitambo ya kufanyia kazi fulani. Vyombo vingine ni vikubwa na vingine ni vidogo. Jembe la mkono, ni chombo cha kufanyia kazi ya kulima. Plau ya ng'ombe ni chombo kikubwa; na trakta ni chombo kikubwa zaidi. Lakini vyote hivi ni matokeo ya juhudi ya binadamu, na kwa kweli ni mali ya wafanyakazi.

Vitu hivi ni vya lazima sana kwa uchumi na maendeleo ya binadamu. Njia rahisi kabisa ya kumwezesha mtu mmoja kuishi kwa jasho la watu wengine ni kumwachia amiliki vitu hivi au baadhi yake. Mtu mmoja angeweza kusema ardhi yote ya kijiji chenu ni mali yake, ni dhahiri kwamba ninyi wengine wote mkitaka kuvitumia sharti mpate idhini yake. Na yeye hawezi kuwapeni ardhi bure; lazima mumlipe kodi ya kutumia ardhi "yake". Na kwa kweli zamani huu ndio ulikuwa msingi mkubwa wa unyonyaji duniani. Hata siku hizo kuna nchi nyingi ambazo makabaila wengi wanamiliki ardhi na wanaitumia kunyonya damu za watu maskini.

Kadhalika majembe yote yangekuwa ni mali ya mtu mmoja, mtu huyu atapata uwezo mkubwa sana wa kunyonya wenzake. Mkitaka kulima sharti mkaazime majembe kwake; na ni dhahiri kwamba hawezi kuwaazimeni majembe "yake" bure. Atawatozeni ushuru wa kuyatumia. Na siku hizi huu ndiyo mrija mkubwa wa mabepari wote duniani. Tena ni jeuri, hakuazimi jembe. Atakwambia, "Kama unataka kulima njoo ulime katika shamba langu nami nitakulipa mshahara; lakini sikubali kukuazima jembe langu ukalimie shamba lako mwenyewe". Au atakwambia, "Kama unataka kufuma nguo njoo ufume katika kiwanda changu; lakini sikuazimi wewe, wala wewe pamoja na wenzi wako, mitambo yangu mkafumie nguo zenu wenyewe". Huyu anatumia uwezo alio nao wa kumiliki vyombo vya kazi ambavyo ni matunda ya kazi ya binadamu, na ambavyo wala si yeye aliyevitengeneza, kuwanyonyea binadamu wenzake.

Huu ndio unyonyaji wa kibepari. Wakati mwingine bepari na kabaila, yaani mwenye ardhi na mwenye jembe, huwa ni mtu yuleyule au kikundi kile kile; na hapo uwezo wake wa kuwanyonya binadamu wenzake huwa ni mkubwa mno. Ndiyo maana chama chetu kinasema namna ya pekee ya kudumisha ujamaa ni kuthibitisha kuwa njia kuu zote za uchumi wa nchi yetu zinatawaliwa na kumilikiwa na wakulima na wafanyakazi wenyewe.

*Demokrasi*

Azimio la Arusha linasema kuwa nchi haiwi ni ya ujamaa kwa sababu tu njia kuu zote za uchumi zimo mikonomi mwa serikali au vyama vya wakulima na wafanyakazi. Sharti tuichunguze serikali yenyewe. Sharti tuthibitishe kuwa ni serikali ya wakulima na wafanyakazi; na kwamba inachaguliwa na kuongozwa na wakulima na wafanyakazi; na kwamba inafanya kazi kwa manufaa ya wakulima na wafanyakazi; na kwamba viongozi wake wanaweza kubadilishwa na wakulima na wafanyakazi. Kadhalika, hatuna budi tuthibitishe kuwa vyama vya ushirika ni vyama vya wakulima na wafanyakazi; na kwamba vinaundwa na kuongozwa na wakulima na wafanyakazi; na kwamba vinafanya kazi kwa manufaa ya wakulima na wafanyakazi; na kwamba viongozi wake wanaweza kubadilishwa na wakulima na wafanyakazi. Serikali ya kidhalimu ikimiliki mali yote ya nchi itakuwa na uwezo zaidi wa kudhulumu wananchi. Vyama vya wakulima makabaila au mabepari vikimiliki mali yote ya nchi vitadumisha tu unyonyaji. Vyama lazima viwe ni vya wakulima na wafanyakazi wenyewe; na serikali japo ya kijijini, lazima iwe ni ya wakulima na wafanyakazi wenyewe. Chama chetu kinasema hakuna ujamaa wa kweli mahali ambapo hakuna demokrasi ya kweli.

Ndiyo maana chama chetu kimeweka masharti ya uongozi. Katika nchi nyingi duniani mali ni kitu kinachosaidia watu wachache kushika madaraka ya kutawala na kuongoza nchi zao. Viongozi wa nchi za kikabaila mara nyingi ni matajiri, na kama si matajiri sana basi hudhaminiwa na matajiri wakubwa. Nchi hizo japo kweli zinaitwa nchi za demokrasi si za demokrasi ya kweli. Ni kweli kwamba katika nchi hizo uchaguzi wa viongozi hufanywa kila baada ya miaka fulani kupita: kwa desturi huwa baada ya kila miaka minne au mitano.

Ni kweli pia kwamba utaratibu wa uchaguzi ni mzuri na kura hupigwa kwa siri na bila hofu. Ni kweli pia kwamba wapiga kura ni wananchi wote watu wazima.

Lakini ukweli mkubwa zaidi ni kwamba wapigiwa kura ni matajiri au vibaraka wa matajiri ambao pia ni watu wenye mali ya kutosha. Demokrasi hii ni sawasawa na demokrasi ya watazamaji na wachezaji mpira. Ni kweli kila mtazamaji ana uhuru kamili wa kuchagua timu yake. Ni kweli ana uhuru wa kwenda kukaa pembeni mwa kiwanja na kushangilia timu yake mpaka mapafu yake yapasuke. Ni kweli wakati wa mapumziko hata yeye anaweza kuingia kiwanjani. Lakini ukweli ni kwamba wachezaji wanajulikana. Kila klabu imeweka masharti ya uanachama; usipoyatimiza masharti hayo hukubaliwi kuwa mchezaji wa klabu hiyo. Kushangilia hakuna masharti. Mtu yeyote akipenda timu ya klabu yetu naye tunaweza kumfanya mwanachama. Lakini ni mwanachama wa kutoa mchango na kushangilia, siyo mwanachama wa kucheza. Hiyo kwa kweli ndiyo demokrasi ya kikabaila. Kila mtu anao uhuru wa kupiga kura na kushangilia washindi; lakini washindani, hasa wa Amerika, ni matajiri – au wapenzi wa matajiri.

Nchi yetu imefanya kinyume. Katika nchi yetu wapiga kura ni wakulima na wafanyakazi, wapigiwa kura pia ni wakulima na wafanyakazi. Katika nchi yetu mpigiwa kura akigundulika kuwa ana mali atatiliwa mashaka makubwa; ataulizwa ameipataje. Ikigundulika kuwa ameipata kwa njia ya kikabaila atanyimwa kabisa nafasi ya uongozi katika nchi yetu. Ikigundulika kuwa hakuipata kwa kunyonya ataambiwa athibitishe kuwa hataitumia mali yake kunyonya watu wengine na wala hatajiingiza katika shuguli zozote za unyonyaji.

Katika nchi yetu mtu anayetiliwa mashaka ni tajiri. Maskini hatiliwi mashaka, maana maskini ndiyo wengi na ndiyo wenye Tanzania yao, na ndiyo watakaoijenga kwa jasho lao na kuitoa nchi yao na wao wenyewe katika hali ya umaskini. Shabaha yao ni kujenga Tanzania ambayo haina maskini na wala haina tajiri; wanajua kuwa haiwezekani kumfanya kila mtu tajiri; kwa hiyo wakiruhusu utajiri ni wa watu wachache tu watakaokuwa

matajiri, na wala si kwa nguvu zao ila kwa kuwanyonya wenzao. Lakini wanajua kuwa inawezekana kujenga nchi ambayo haina maskini hata mmoja. Na hiyo ndiyo shabaha ya Chama chetu.

*Imani ya Moyo*

Mambo haya ni mepesi kueleza lakini ni magumu kutimiza. Katika nchi zote duniani watu walio wengi zaidi ni wakulima na wafanyakazi. Na kama tulivyokwisha kusema, katika baadhi ya nchi hizo wakulima na wafanyakazi wanayo haki kamili ya kupiga kura. Ni dhahiri kwamba watu hawa wangependa na kunuia kwa dhati kuanzisha na kuongoza serikali ya wakulima na wafanyakazi wangefaulu, japo kwa taabu. Lakini makabaila ni wajanja. Huwaambia wafanyakazi kwamba katika nchi hizo kila kibarua unaweza kuwa tajiri na kabaila. Huwatajia hata majina ya matajiri fulani fulani ambao kwanza walikuwa maskini au baba zao walikuwa maskini. Baadhi ya wafanyakazi wakisikia hivyo, na hasa wale viongozi wao ambao ndiyo wangewaongoza wafanyakazi katika mapinduzi ya kufuta umaskini na ukabaila, hushikwa na tamaa na basi huendelea wakitumaini kwamba huenda siku moja na wao pia watakuwa matajiri. Wanaweza. Lakini wawili watatu tu; si wengi.

Ndiyo maana Chama chetu kinasema kuwa viongozi wetu hawana budi wawe ni watu ambao wanaamini kabisa siasa ya ujamaa. Kama ni watu wanaoikubali na kuiamini kabisa siasa ya ujamaa hawatashawishiwa na makabaila kwa tamaa za kujipatia pato la kunyonya, wawaache wafanyakazi na wakulima wenzao na kwenda kwa makabaila. Kama wanakubali na kuamini kabisa siasa ya ujamaa uongozi wao hautakuwa wa kuwasaidia makabaila na mabepari bali uongozi wao utakuwa ni wa kuwasaidia wakulima na wafanyakazi katika mapinduzi yao ya kutokomeza ukabaila na umaskini. Kama wanakubali na kuamini kabisa siasa ya ujamaa watafanya kila jitihada kuielewa zaidi na kufanya kila wawezalo kuona kuwa imefaulu. Kama wanakubali na kuamini siasa ya ujamaa, watavumilia kila gumu watakalokutana nalo; na kila mara watajiandaa kuvumilia magumu zaidi

kusudi siasa ya ujamaa ifaulu katika nchi yetu. Ujamaa ndiyo utu. Mtu kumnyonya mtu ni dalili ya ushenzi na unyama. Viongozi wetu wakikubali na kuamini siasa ya ujamaa na kutambua kuwa msingi wake ni utu na usawa wa binadamu, watakuwa tayari hata kutoa maisha yao wenyewe ili kuona kuwa siasa ya ujamaa inafaulu katika nchi yetu.

Hii ndiyo imani ya Chama chetu. Si ndogo, ni kubwa. Si nyepesi, ni nzito; si rahisi kutimizwa ni ngumu. Lakini ndiyo imani ya utu. Ndiyo inayoweza kututoa wote pamoja katika unyonge tuliorithi.

Azimio la Arusha linasema: Tumeonewa kiasi cha kutosha, tumenyonywa kiasi cha kutosha, na tumepuuzwa kiasi cha kutosha. Unyonge wetu ndiyo uliotufanya tuonewe, tunyonywe na kupuuzwa. Sasa tunataka mapinduzi; mapinduzi ya kuondoa unyonge wetu, ili tusionewe tena, tusinyonywe tena, na wala tusipuuzwe tena.

Mapinduzi haya yanayotakiwa ni kwa wote, si kwa wachache. Tulipoonewa, tulionewa wote; tuliponyonywa, tulinyonywa wote; tulipopuuzwa, tulipuuzwa wote. Ni unyonge wetu sote kwa pamoja ndiyo uliofanya tukaonewa, tukanyonywa, na tukapuuzwa. Mapinduzi tunayotaka sasa ni lazima yawe ni yetu wote pamoja, ili Mtanzania yeyote asiwe mnyonge, na unyonge wake ukatumiwa kumnyonya na kumpuuza. Ni aibu kwa kiongozi wa TANU na Serikali yetu kutafuta njia ya mkato ya kujitoa yeye peke yake katika unyonge wa kuonewa, kunyonywa na kupuuzwa na kuwaacha Watanzania wengine katika hali hiyo hiyo. Na ni dhambi kwa kiongozi yeyote wa Chama chetu na Serikali kuwa chombo cha wale ambao jana walitufanya wanyonge ili watuonee, watunyonye, na kutupuuza, kusudi hata leo waendelee kutuonea, kutunyonya na kutupuuza.

Hiyo ndiyo imani ya Chama. Ndiyo tunayotaka iwe msingi wa mawazo na maneno na matendo ya Wanachama na viongozi wetu popote walipo. Ndiyo imani peke yake itakayotuwezesha kujenga Tanzania ambayo kila Mtanzania ataweza kujivunia.

Inataka watu wanaoikubali.